Jumatano Januari 24, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581565

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



**UNITED YATOA OFA KUWAUZA ANTHONY NA SANCHO SAUDIA**

UKURASA 22

# Polisi, CHADEMA wafikia mwafaka

• **Ni** kuhusu maandamano ya 'amani' Dar, ulinzi kuimarishwa... *Endelea ukurasa 2*



Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe



Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM, Paul Makonda



Kamanda wa Kanda Maalumu, Jumanne Muliro

## NEMC yafafanua povu lililodhaniwa kuwa la muujiza



UKURASA 3

**ACT**- Wazalendo yataja mwarobaini maafa mafuriko



UKURASA 3

**Utajiri** wa Mo Dewji wazidi kupaa Afrika



UKURASA 4

**Wataka** jinsia kuwa lazima uteuzi wagombea

UKURASA 4



Rais Samia Suluhu Hassan alipokuwa China

## Ziara ya Rais Samia China yaleta neema sekta ya afya

UKURASA 2

**MICHEZO** TAIFA STARS MACHOZI, JASHO NA DAMU LEO UK.24 **KATUNI** UK.6




Ndege aina ya 'Marabou stork' maarufu 'Bwana Afya' au mwarabu, wakiwa pembezoni mwa mwalo katika Feri ya Kamanga, Ziwa Victoria, jijini Mwanza, jana. Ndege hao ni maarufu kwa kula uchafu utokanao na samaki.
**PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Polisi, CHADEMA wafikia mwafaka maandamano

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kupitia kwa Katibu Mkuu wake, John Mnyika, jana kilithibitisha kupokea barua ya kutoka kwa Jeshi la Polisi ya kuruhusiwa kufanya maandamano ya amani.

Nipashe lilifanikiwa kuona barua ambayo iliandikwa jana na kusainiwa na Mkuu wa Polisi Kariakoo ya kutoa ruhusa kwa chama kufanya maandamano hayo.

"Kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zinazohusu taarifa za maandamano, hayatazuiwa na Jeshi la Polisi iwapo hayataleta uvunjifu wa amani au kusababisha kutendeka kwa vitendo vya kihalifu," ilisomeka sehemu ya barua hiyo.

Kwa mujibu wa Mnyika, chama hicho kilipeleka barua ya taarifa ya maandamano hayo katika ofisi mbalimbali za polisi wilaya.

"Kuna barua moja imeletwa wakati mimi tayari nimeshatoka ofisini na nimeomba wanisomee, na inaonyesha kwamba imetoka kwa Jeshi la Polisi Kariakoo, na wameruhusu maandamano, kwa hiyo kikubwa ni kwamba maandamano yameruhusiwa," alisema Mnyika, alipoongea na Nipashe kwa simu.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Murilo, alipotafutwa kwa njia ya simu kuthibitisha kuruhusu maandamano hayo, simu yake haikupokewa na alipotafuwa tena haikupatikana hewani.

CHADEMA imesema inafanya maandamano kushinikiza serikali kuondoa bungeni miswaada inayohusu vyama vya siasa na uchaguzi.

Baadhi ya vipengele vinavyokosolewa na chama hicho kwenye miswada hiyo mitatu ambayo tayari imewasilishwa bungeni ni pamoja na tume huru ya uchaguzi.

Barua iliyosambaa mtandaoni yenye kumbukumbu namba GB.795/1054/01/03 ya Januari 23, yenye kichwa cha habari "Yahusu taarifa ya maandamano" ilisema wanarejea barua yenye Kumb No. C/ADM/MS/11/59 ya Januari 16, mwaka huu.

"Kwa barua hii viongozi wa CDM (CHADEMA) na wanachama mnalo jukumu la kuzuia lugha za uchochezi, kejeli, zinazoweza kupelekea kutendeka kwa vitendo vya uvunjifu wa sheria. Mtalazimika kufuata utaratibu wa kisheria katika maeneo yote kwa kadri mtakavyoelekezwa na wasimamizi wa sheria, polisi wakiwa ni kiongozi katika eneo hilo mlilotolea taarifa,"

"Maandamano hayo yasisababishe uvunjifu wa amani/watu kuibiwa au kuporwa na yawe kwenye njia zilizokubaliwa. Taarifa yenu izingatie muda wa kilichoelezwa kwenye barua yenu ikiwa ni pamoja na kutoanzishwa mambo mengine ambayo hayamo kwenye taarifa iliyotolewa polisi.

"Aidha, ukiukwaji wowote wa masharti hayo utalilazimisha jeshi la polisi kuchukua hatua za kisheria bila kusita ili kuzuia madhara ya kuvunjika kwa amani. Naamini msingi wa taarifa yenu utabaki kuwa ni kudumishwa kwa amani na utulivu uliopo nchini."

**KAULI YA MAKONDA**

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, amemshauri Mwenyekiti wa Chama Cha Demokrasia (CHADEMA), Freeman Mbowe, kurudi katika meza ya maridhiano ambayo ni msingi wa amani wa taifa na maendeleo, badala ya kukimbilia Umoja wa Mataifa (UN) kutangaza nchi vibaya.

Akihutubia wananchi wilayani Hai, Mkoa wa Kilimanjaro kwenye mwendelezo wa ziara yake ya mikoa 20 ya kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi na kutatua kero za wananchi, alisema anashangazwa na mwenyekiti huyo kukiuka makubaliano yao.

"Yaani Kaka yangu Mbowe, linapokuja suala la fedha na kuomba michango kwa viongozi wa serikali anakubali maridhiano, tunapokuja ajenda za umoja wa kitaifa tukamwambia maridhiano bado anakimbilia Ulaya hii sio sawa," alisema Makonda na kuongeza;

"Mbowe anakubali fedha za michango ya Rais Samia Suluhu Hasssan, kwanini hataki kuridhiana katika mambo ya umoja wa kitaifa yanayoleta amani, kama Rais Samia alisikia kilio akamtoa kule ndani bila kuwa na wazungu, nini kinashindikana kukaa mezani na mambo yakaenda sawa," alihoji.

Alisema maandamano wanayotaka ni kuvuruga biashara za watu, wagombane, waonekane wanazuiliwa na wapate picha ili waende nje ya nchi kuomba fedha.

Makonda alisema, Rais Samia amefanya mambo mengi kwa viongozi wa upinzani, ikiwamo kuwatoa gerezani na kuwaita Ikulu katika maridhiano, na kwamba haipendezi kuona wanamgeuka kipindi hiki.

"Sio vizuri kuchezea amani tuliyonayo kwani yako mataifa yana tamani kuona hii nchi inavurugika, wanatamani kuona ina migogoro jambo ambalo hatuwezi kukubali tupo tayari kuingia katika maridhiano," alisema Makonda.

"Kaka yangu Mbowe nampenda na hilo analijua ni miongoni mwa watu ambao ninawaheshimu, maandamano tangu lini yakapelekwa UN, yaani ulalamikie wabunge mswada utolewe bungeni halafu badala ya kwenda kule unakimbilia UN...," alihoji.

Alisema, mafanikio na maendeleo ya Chadema yanatokana na matunda ya Rais Dk. Samia kuwawezesha kifedha kwa kuwalipa malimbikio ya ruzuku.

Aidha, aliwasihi wakazi wa Kilimanjaro kumuunga mkono Rais Dk. Samia ambaye mekuwa akiwapatanisha Watanzania bila kujali chama, kabila wala kipato na kila aliyemwendea na kulalamika alimsikiliza na kuchukua hatua.

***Imeandaliwa na Elizabeth Zaya (DAR) na Beatrice Shayo (HAI)**

## Ziara ya Rais Samia China yaleta neema sekta ya afya

**Na Mwandishi Wetu**

ZIARA ya Rais, Samia Suluhu Hassan nchini China Novemba, 2022, imeendelea kuzaa matunda baada ya Naibu Waziri Mkuu wa taifa hilo, Liu Guozhong, kutua nchini na kuahidi uwekezaji katika viwanda vya vifaa tiba na dawa kwenye viwanda vya ndani.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati Guozhong alipotembelea Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema kuna maeneo watakayoshirikiana na China, ikiwamo upatikanaji wa vifaa tiba vya moyo katika viwanda nchini ili kupunguza gharama za matibabu.

Dk. Mollel alisema katika ziara yake hiyo juzi, Guozhong alitembelea chumba cha upasuaji mdogo wa moyo, chumba cha wagonjwa wa moyo wanaohitaji uangalizi maalum na chumba cha uangalizi maalum kwa wagonjwa waliofanyiwa upasuaji wa moyo.

"Ziara ya Guozhong nchini Tanzania ni sehemu ya uhusiano mzuri baina ya Tanzania na China. Haya ni matunda ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini China hivi karibuni na ni mapinduzi makubwa yaliyofanywa na Rais wetu huyo katika kuwekeza kwenye sekta ya afya, hususani Tiba Utalii," alisema Dk. Mollel.

"Ushirikiano wetu na China ni kubadilishana ujuzi katika kutoa huduma kwa wananchi, ikiwa ni sehemu ya kujitanua zaidi eneo la tiba utalii," alisisitiza.

Guozhong alisema ushirikiano wa Tanzania na China ni sehemu ya kuendeleza undugu wa kihistoria uliopo baina ya mataifa hayo tangu zamani.

"Kwa niaba ya serikali ya China, tutahakikisha ushirikiano wetu huu na Tanzania katika sekta hii ya afya, unakuwa na tija kama sehemu ya kuenzi undugu wa kihistoria wa baina ya mataifa haya mawili," alisema.

Guozhong jana alitembelea Makumbusho ya Taifa na Nyumba ya Sanaa kabla ya kukutana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ofisini kwake, Magogoni jijini Dar es Salaam.

Pia alikutana na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, katika ofisi za Wizara ya Madini, jijini Dar es Salaam.

Katika ziara hizo, Naibu Waziri Mkuu Guozhong alifanya mazungumzo na viongozi hao yanayohusiana na masuala ya ushirikiano katika sekta mbalimbali baina ya Tanzania na China.

Ziara ya Rais Dk. Samia nchini China, Novemba, 2022 kutokana na Mwalimu wa mwenyeweji wake, Rais Xi Jinping, iliweka rekodi kwa kuwa ya kwanza kufanywa na kiongozi wa juu kutoka Bara la Afrika, tangu Rais Xi alipochaguliwa tena na Mkutano Mkuu wa 20 wa Chama cha Kikomunisti cha China.

HABARI KITAIFA

# NEMC yafafanua povu lililodhaniwa la muujiza

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Morogoro na Pwani, limefafanua kuhusu taharuki iliyoibuka mjini hapa Jumamosi iliyopita baada ya kunyesha mvua kubwa ya upepo na radi hatimaye kuonekana povu kubwa jeupe likisambaa kwenye vijito vya maji.

Kutokana na taharuki hiyo, baadhi ya watu waliibuka na mitazamo tofauti ikiwamo ya kuanguka kwa mawingu au miujiza.

NEMC katika taarifa yake jana, ilisema si kweli kwamba ni miujiza au mabadiliko ya tabia nchi wala wingu kama ambavyo wengi walifikiri.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, uchunguzi uliofanywa na wataalamu wa baraza hilo kwa kushirikiana na wale wa Bonde la Wami Ruvu na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, umebaini kuwa chanzo cha povu hilo ni kumwagika kwa kemikali yenye tabia kama ya sabuni ambayo haijafahamika mara moja lakini inatoa povu jingi na kali maradufu zaidi ya sabuni ya kawaida.

Meneja wa NEMC Kanda ya Morogoro na Pwani, Abel Sembeka, alisema wataalamu hao wamefanya uchunguzi wa awali na kugundua hali hiyo iliyoonekana zaidi maeneo ya Area Six B, Kola A na Kata ya Tungi haikusababishwa na mabadiliko ya tabia nchi.

"Kupasuka kwa madumu mawili yaliyokuwa yamebeba kemikali hiyo iliyokuwa ikisafirishwa kutoka Dar es Salaam kwenda mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hadi nje ya nchi, ndicho chanzo cha kutokea kwa hali hiyo," alisema Sembeka.

Meneja huyo licha ya kubainisha kemikali hiyo yenye tabia kama ya grisi kuwa ilikuwa ikisafirishwa kwenye lori lenye namba za usajili T 623 EEA mali ya kampuni ya R.J Motchand, alisema bado wanaendelea na uchunguzi na kusubiri majibu kutoka ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kujua aina ya kemikali hiyo na madhara yake ya muda mfupi, wa kati na muda mrefu kwa viumbe hai na mazingira.

Alisema dereva wa lori hilo baada ya kugundua ajali hiyo iliyotokea Januari 14 wakati akitokea Dar es Salaam kwenda mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwenda nje ya nchi, alisimama kwenye maegesho ya malori eneo la Area Six na kupakia upya ili kuendelea na safari. Lakini wakati akiendelea kufanya hivyo, alisema kemikali nyingine ilimwagika chini na kusambazwa na maji na upepo.

Sembeka aliwatoa hofu wananchi kuwa hadi sasa hakuna majani yoyote yaliyoungua eneo la tukio wala kuonekana kiumbe chochote kilichokufa ingawa alitaja athari kubwa za kemikali za aina hiyo kusababisha michubuko kwa ngozi kuchunika na ukali wa kemikali za aina hiyo. Aidha, alihadharisha kama kuna wananchi waliochukua kemikali hiyo kwa nia ya kuitumia kama sabuni, kuachana na matumizi hayo kwa sababu si kwa ajili ya matumizi ya nyumbani bali ni viwandani.

Meneja huyo alibainisha kuwa kemikali hiyo ilikuwa ikipelekwa migodini kwa ajili ya kusafishia madini au kemikali zilizoko kwenye maeneo hayo.

"Niwatahadharishe tu wananchi, likitokea gari limemwagika kemikali kwa bahati mbaya, mtu yeyote asiichukue na kupeleka nyumbani kwani ni hatari kwa usalama wa afya," alisema.




Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (kulia) na Msuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za kodi, Roberty Manyama wakifungua pazia jijini Dodoma jana, kuzindua rasmi tovuti ya Taasisi ya Usuluhishi wa malalamiko ya taarifa za kodi nchini (TOST), itakayosaidia kupokea malalamiko ya kikodi nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# ACT-Wazalendo yaja na mwarobaini maafa mafuriko

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimeomba serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), kutoa misaada ya kibinadamu kwa wananchi walioathiriwa na mafuriko nchi nzima.

Chama hicho kimetoa kauli hiyo baada ya kunyesha mvua na kuathiri baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam na mikoa mingine.

"Tahadhari ya uwapo wa mvua kubwa ya kuleta madhara ilishatolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) Julai, mwaka jana. ACT-Wazalendo kila mara tulifanya wajibu wa kuzikumbusha mamlaka za serikali kuchukua tahadhari ya jambo hilo kwa ajili ya kuzuia madhara yasiwe makubwa," alisema Dorothy Semu, Makamu Mwenyekiti ACT-Wazalendo.

"ACT-Wazalendo tumesikitishwa na kauli za viongozi wa nchi zinazolenga kuwalaumu wananchi kwa madai kwamba wamejenga maeneo ya bondeni. Ushahidi wa matukio ya mvua umeonyesha imeathiri maeneo mengi ambayo kwa asili siyo ya bondeni, kama vile janga la Kateshi Hanang, Kagera, Nachingwea, Songwe, Arusha mjini na baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam kama vile Kinondoni, Kunduchi, Tegeta."

Dorothy alisema mafuriko katika Jiji la Dar es Salaam hayasababishwi na watu kujenga mabondeni pekee, chanzo kikubwa ni kukosekana kwa mifumo ya kuondosha maji ya mvua jukumu linalopaswa kusimamiwa na serikali.

Aliitaka serikali kuunda kamati ya pamoja ya kukabiliana na majanga itakayohusisha TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mamlaka ya Hali ya Hewa, ili kufuatilia hatua mbalimbali za kukabiliana na janga hilo kwa ngazi za wizara za kisekta, mamlaka za serikali za mitaa na wananchi.

Kadhalika, aliitaka Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na TAMISEMI, zifanye ukarabati na matengenezo ya miundombinu iliyoharibiwa na mvua ili kurejesha mawasiliano na uchukuzi, kufanya marejeo ya mipangomiji na kutengeneza mkakati wa muda mrefu na wa kati wa ujenzi wa mitaro mikubwa ya kupitisha maji mengi nyatakati za mvua.

Aliitaka TAMISEMI kuunda timu ya wataalam wa mipangomiji ili ipitie maeneo yote ya Mkoa wa Dar es Salaam na kuangalia waliojenga kwa mtindo wa kuhatarisha makazi mengine, waliowekewa uzio maeneo bila ya kuyaendeleza na ambao wamejenga maeneo hatarishi.

Pia, baada ya kufanya hivyo, wanatakiwa wakabidhi ripoti kwa mamlaka husika ili serikali ije na mpango rafiki wa kuboresha na kutengeneza namna bora ya kujikinga na majanga hayo.

IOGT·NTO·MOVEMENT

## Publication of Bi-Annual Income and Expenditure

**IOGT-NTO Movement** is a Swedish organization, registered in Tanzania as an International NGO, addressing the alcohol harm in Tanzania, Kenya, Rwanda, and Uganda. IOGT-NTO Movement works through local partner organizations to fulfil its goal to create strong communities where people are empowered, rights are protected and harm from alcohol and other drugs is minimized.

**Our Vision:** A democratic world characterized by solidarity and equality where alcohol and other drugs do not impede peoples' welfare, freedom and security.

**Our Mission:** To strengthen relevant actors in their work for reduced use of alcohol and other drugs in developing countries and thus contribute to democratic development, strengthen rights and reduced poverty.

| Bi-Annual Income and Expenditure Report for the Period of July to December 2023. | |
|---|---|
| **Income:** | |
| Balance Brought forward plus Receipt from Donors | 157,104,639 |
| **Expenditure:** | |
| Human Resource | 82,281.799 |
| Office Administration and Communication | 6,124,373 |
| Capacity Development and Networking | 15,532,963 |
| Quality and Compliance Monitoring | 44,046,099 |
| Planning Meetings | 203,500 |
| **Total Expenditure** | **150,188,734** |

IOGT NTO Movement - East Africa Office
Plot No. 43, Uporoto Street
Box 7522, Dar Es Salaam Tanzania
eaoffice@iogtntomovement.se
www.iogtntororelsen.se/

VISIT FREE ENTRY
INTL TRADE EXHIBITION ON FOOD & PROCESSING PLASTICS & PACKAGING

EXHIBITORS FROM AROUND 13 COUNTRIES

FOODPACK 2024
INTL FOOD & PROCESSING TRADE SHOW - EAST AFRICA

Products on Display:
Juices | Refrigeration Systems | Storage Displays | Bakery Ingredients
Oil Seeds | Agro Commodities | Tea | Milk | Diapers | Rice

INTERPLAST-PACK 2024
INTL TRADE EXHIBITION ON PLASTICS, POLYMERS, RUBBER, CORRUGATED PACKAGING & PRINTING

Products on Display:
Paper | Disposable Packaging Machinery | Plastic Raw Material
Polypropylene | Woven Products

Date & Venue
26-28 January 2024
Diamond Jubilee Hall, Dar-Es-Salaam - Tanzania

Timing
10:00 AM TO 6:00 PM

For more info, Please Call
0768 616 418 / 0656 482 557

# Utajiri Mo Dewji waongezeka, aking'ara na mabilionea Afrika

Na Mwandishi Wetu

UTAJIRI wa mfanyabiashara maarufu nchini, Mohammed Dewji 'Mo', umeongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 1.5 mwaka jana hadi Dola bilioni 1.8 mwaka huu, kwa mujibu wa ripoti mpya ya Jarida la Forbes.

Katika orodha yake mpya ya mabilionea barani Afrika, Forbes imemtaja Mo Dewji, Rais wa kundi la kampuni za Mohammed Enterprise Tanzania Ltd (MeTL Group), kuwa amepanda hadi nafasi ya 12 kutoka nafasi ya 13 ya orodha ya mabilionea barani Afrika aliyokuwa akishika mwaka jana.

Katika orodha hiyo, Mo Dewji ameendelea kubaki kuwa bilionea pekee kijana kwa miaka 10 mfululizo akiwa na umri wa miaka 48 na ni bilionea pekee kutoka ukanda wa Afrika Mashariki na Kati ambaye amepenya kwenye orodha hiyo mpya ya mabilionea.

Kwa mujibu wa Forbes, mfanyabiashara huyo wa Kitanzania ametengeneza ajira kwa watu 40,000 kutoka ajira 35,000 za mwaka jana. Mo Dewji ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni za METL, zilizoanzishwa na baba yake miaka ya 1970.

METL ni wazalishaji wa bidhaa nyingi zikiwano unga, nguo, vinywaji na mafuta katika mashariki na kusini mwa Afrika pia Afrika ya Kati. Mbali na Tanzania, METL inafanya shughuli zake za biashara katika nchi 10 barani Afrika zikiwamo Uganda, Ethiopia na Kenya.


Katika orodha ya mabilionea 20 Afrika wa mwaka 2024, Forbes imebainisha kuwa matajiri hao wana mali zenye thamani ya jumla ya Dola za Marekani bilioni 82. Ni ongezeko la Dola milioni 900 kutoka utajiri Dola bilioni 81.5 za mwaka jana.

Orodha ya Forbes inaonyesha kuwa Aliko Dangote bado anashika nafasi ya kwanza akiwa na utajiri wa Dola za Marekani bilioni 13.9 akifuatiwa na Johann Rupert & family kwa Dola bilioni 10.1.

Wengine na ukwasi wao wa dola za Marekani kwenye mabano ni Nicky Oppenheimer (bilioni 9.4), Nassef Sawiris (bilioni 8.7b), Mike Adenuga (bilioni 6.9), Abdulsamad Rabiu (bilioni 5.9), Naguib Sawiris (bilioni 3.8b), Mohamed Mansour (bilioni 3.2b), Koos Bekker (bilioni 2.7), Patrice Motsepe (bilioni 2.7), Issad Rebrab & family (bilioni 2.5b na Strive Masiyiwa (bilioni 1.8b).

Katika orodha hiyo pia wamo Aziz Akhannouch & family (bilioni 1.7), Othman Benjelloun & family (bilioni 1.4b), Youssef Mansour (bilioni 1.3), Yasseen Mansour (bilioni 1.2b, Christoffel Wiese (bilioni 1.2), Michiel Le Roux na Femi Otedola dola bilioni 1.1 kila mmoja.

Hata hivyo, Afrika inatajwa kuwa bara gumu kiuwekezaji kutokana na changamoto mbalimbali ukiwamo ubovu wa miundombinu, huku utashi wa kisiasa kusaka mabadiliko ukileta matumaini katika baadhi ya nchi.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Msingi Mapinduzi, alipofanya ziara wilayani Serengeti juzi, kuangalia hali halisi ya upokeaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza. Kulia Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Muta Charles. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfanyakazi wa bomba la mafuta akutwa amefariki

Na Shaban Njia, KAHAMA

MFANYAKAZI wa bomba la mafuta na Mkazi wa Mtaa wa Nyasubi, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, Ahmed Ally (56), amekutwa ameuawa na watu wasiojulikana nyumbani kwake kisha kuacha wamemfungia kwa nje.

Akisimulia tukio hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Nyasubi, Leonard Mayala, alisema taarifa za kutokea kwa kifo hicho alizipata kwa majirani ambao Ally alikuwa amepanga nao sehemu moja baada ya kusikia harufu mbaya.

Mayala alisema alifika kwenye eneo la tukio na kukuta mlango umefungwa kwa nje na harufu ikitokea dirishani, ndipo walipotoa taarifa Kituo cha Polisi cha Kahama, ambao walikwenda kuvunja mlango na kukuta mwili wa mfanyakazi huyo umeanza kuharibika.

Baadhi ya mashuhuda na majirani wa marehemu, akiwamo Dumisha Kabaula, alisema mtu huyo alitokea Dar es Salaam kuja Kahama kufanya kazi, lakini siku kadhaa bila kwenda kazini na alipomwuliza alidai anaumwa, na siku hiyo alikuwa ajiandaa kuhama lakini baada ya siku nne wakapata taarifa za kifo chake.

Valentina Joseph alidai alikutana na Ally macho yakiwa mekundu tofauti na alivyomzoea na alipomuuliza juu ya hali hiyo alijibiwa kuwa anaumwa hivyo anataka kupumzika.

"Tangu siku hiyo hakuwahi kutoka ndani hadi Januari 20, mwaka huu, tulipoanza kusikia harufu kali na mlango ukiwa umefungwa kwa nje.

Mmiliki wa nyumba aliyekuwa amepanga Ally, Michael Kamori, alisema mkataba wake ulikuwa umeshakwisha wa kuendelea kuishi kwenye nyumba hiyo na aliomba kuongezewa muda hadi Januari 20, mwaka huu, atakuwa ameshapata sehemu nyingine na kuondoka na badala yake amepata taarifa ya kifo chake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuwa mwili wake ulikuwa umeanza kuharibika akibainisha chanzo cha tukio hilo kuwa bado hakijafahamika na wanaendelea na uchunguzi.

Alisema mwili ulichukuliwa na kupelekwa katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama kwa uchunguzi zaidi na baadaye walikabidhi kwa ndugu zake kwa ajili ya mazishi.

Aidha, Kamanda Magomi alisema mpaka sasa hakuna mtu yeyote anayeshukiwa juu ya tukio hilo na wanaendelea na uchunguzi kuwabaini wahusika.

Magomi pia alisema mkazi wa Kata ya Nyihogo, Mariamu Robert (28), alikutwa amejinyonga chumbani kwake akiwa amejifungia ndani na polisi walifika na kuvunja mlango na kumtoa. Chanzo cha tukio hilo pia hakijafahamika na wanaendelea na uchunguzi.

"Kujichukulia sheria mkononi ni kukinzana na sheria kwamba hakuna mtu aliyepo juu ya sheria na kila mmoja anahaki ya kuishi. Niwatake wananchi mkoani hapa hatutasita kumchukulia hatua za kisheria wale wote wanaobainika kujichukulia sheria mkononi ama kwa kuua au kumjeruhi mtu," alisema ACP Magomi.

# Washauri uteuzi kuzingatia jinsia

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAKATI Kamati ya Bunge, Katiba na Sheria ikiendelea na uchambuzi wa maoni ya wadau kuhusu miswada ya sheria za uchaguzi na siasa, wabunge vinara wa masuala ya jinsia wamependekeza Sheria ya Vyama vya Siasa kuweka kifungu cha sheria kitakacholazimisha vyama kufanya uteuzi wa wagombea katika uchaguzi wa chama na serikali kwa kuzingatia jinsia.

Aidha, wamependekeza kuwekwa kifungu cha kuwaengua wagombea watakaobainika kufanya unyanyasaji wa kijinsia.

Miswada hiyo ni Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023, Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023 na Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2023.

Akizungumza kwenye kikao cha kujadili sheria hizo, Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangira, alisema ili msajili apate neno la kusimamia katika sheria ya vyama vya siasa, inapendekezwa kuwekwa kifungu cha Sheria ya Vyama vya Siasa kufanya uteuzi wa wagombea katika chaguzi za chama na serikali kwa kuzingatia jinsia.

"Msajili wa vyama vya siasa apate meno ya kusimamia kifungu hiki tunapendekeza kirekebishwe na kuweka asilimia na viwango vya wagombea wanawake," alisema.

Pia alisema wanapendekeza wagombea wanawake wawe angalau asilimia 50 kwenye uchaguzi wa ndani ya chama, wagombea wanawake angalau asilimia 30 kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na wagombea wanawake angalau asilimia 20 kwenye uchaguzi mkuu.

Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko alisema wanawake wengi wamekuwa hawaingii katika siasa kutokana na lugha za unyanyasaji zinazojitokeza kwenye kampeni au uchaguzi wa ndani ya chama.

"Tunapendekeza iwapo mgombea au timu yake ya kampeni anatoa maneno ya kashfa ama kumkosea heshima mgombea mwenzake basi aweze kupoteza sifa ya kugombea. Hata timu ya kampeni na hata chama cha siasa ambacho kimempendeza kiweze kuchukuliwa hatua stahiki," alisema.

Mbunge wa Sikonge, Joseph Kakunda, alisema wameweka utaratibu wa kuanzia na asilimia 30 ili kufikia usawa wa kijinsia bungeni na pia utekelezaji wake unatakiwa kusimamiwa na sheria ambayo itatoa usawa katika kugombea, vikwazo, kuondoa unyanyasaji, dharau, kebehi ambayo mara nyingi yamekuwa yakiwakwaza wanawake.

Alisema wanawake wengi kwa kuogopa kudhalilika kwa maneno wanayoambiwa na baadhi ya watu katika jamii wakati mwingine hata wanawake wenzao ni muhimu kuondoa vikwazo hivyo.

Akifungua kikao, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mary Chatanda, aliwataka wabunge hao kufanya ushawishi wa kutosha kwa wenzao ili muswada huo utakapofika bungeni ili kwenda kwa pamoja katika jambo hilo la kuongeza ushiriki wa wanawake katika siasa.

# Hoja za maandamano kutofanyiwa kazi

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala, Katiba na Sheria, Dk. Joseph Mhagama, amesema maoni yatakayofanyiwa kazi wakati wa kutungwa sheria za uchaguzi ni yale yalitolewa na wadau mbele ya kamati yake na si maandamano ya wanasiasa.

Dk. Mhagama alibainisha hayo jana kwenye viwanja vya Bunge, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu miswada minne ya sheria za uchaguzi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Alisema sheria za uchaguzi zinazaofanyiwa marekebisho au kutungwa hazitazingatia maandamano yaliyopagwa kufanywa na vyama vya siasa bali maoni ya wadau waliyotoa mbele ya kamati hiyo.

"Bunge linafanya kazi kwa kuzingatia maoni yanayotolewa na wabunge, wadau kwenye kamati za Bunge kwa hiyo kwa nafasi hiyo maana yake kamati ya Utawala Katiba na Sheria ndiyo yenye jukumu," alisema Dk. Mhagama.

Aidha, alisema maneno ambayo yanatolewa hivi sasa na viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kuwa maoni yao waliyotoa kuhusu miswada ya sheria za uchaguzi yametupwa ni siasa za maji taka.

"Viongozi wa CHADEMA wote wakubwa wamekuwa wabunge humu tena kwa muda mrefu kuliko mimi Tundu Lissu (Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA) ni mwanasheria mbobezi anawezaje kusema maoni yao yametupwa wakati kamati bado ipo kwenye uchambuzi," alisema.

Alisema kamati hiyo ikishamaliza uchambuzi itarudi na kufanya wasilisho bungeni ambapo Watanzania watajadili pale ambapo itakuwa imetungwa sheria ndipo CHADEMA wanaweza kusema maoni yao yametupwa.

"Kwahiyo mimi niseme ni siasa ya maji taka huwezi kusema maoni yametupwa wakati yapo kwenye uchambuzi halafu hajafika kwenye Bunge na hawa wote wanajua," alisema Mhagama.

Pia alisema viongozi wa CHADEMA, kwa namna ambavyo walivyokuwa wakiwasilisha maoni yao ni kama walikuwa wamejipanga kuharibu mchakato wa kupokea maoni za sheria za uchaguzi.

"Mnyika alivyopewa nafasi ya kutoa maoni ya chama chake kuhusu miswada hii kwanza alianza kuleta hoja ya katiba mpya, lakini nilimwelekeza kujikita kwenye sheria za uchaguzi hivyo ni watu ambao kama walijipanga kutaka kuharibu mchakato wa miswada hii.

"Hivyo niwaombe Watanzania tujikite kwenye miswada ya sheria za uchaguzi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi zitakazopanua demokrasia ya nchi yetu zitakazotoa fursa kwa kinamama kushiriki uchaguzi, wetu kushiriki kwenye uchaguzi, ili kupata viongozi ambao wanatakiwa na wananchi na siyo kulazimisha mambo ambayo yapo nje na mfumo," alisema. Mhagama alisema bunge lipo tayari kushirikina na wametoa ushirikiano mkumbwa na ni kwa mara ya kwanza kamati hiyo imekaa siku nne kupokea maoni kwa wadau wasiopungua 1,707 hali ambayo haijawahi kutokea na itachukua muda mrefu kujirudia.

Kadhalika, akizungumzia kuhusu madai ya CHADEMA, kunyimwa nafasi ya kutoa maoni yao alisema hakuna mdau ambaye alinyimwa fursa hiyo.

Alisema, taasisi za dini zilipewa muda wa dakika 30 kuwasilisha maoni yao na vyama vya siasa vilipewa dakika 20, mashirika dakika 10 na mtu binafsi dakika tano.

Hivi karibuni, Katibu wa CHADEMA, Mnyika alieleza vyombo vya habari kuwa kamati hiyo imekataa kupokea maoni ya maandishi ya chama hicho, pia msimamo wa kufanya maandamano uko pale pale.

# Miili ya Watanzania waliofariki dunia Septemba kuwasili nchini

**Na Elizabeth Zaya**

MIILI ya Watanzania watatu waliofariki dunia Septemba mwaka jana, kwenye ajali ya moto Afrika Kusini, inatarajiwa kurejeshwa kesho nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Balozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini, James Bwana, Watanzania hao waliopoteza maisha ni Said Mohames Kisarazo, Ibrahim Mohamed Kisarazo na Mohames Ismail Amiri.

"Ubalozi unawaarifu kuwa Januari 20, mwaka huu, miili ya Diaspora watatu waliofariki (dunia) kwa ajali ya moto Agosti 31, 2023 jijini Johannesburg, Afrika Kusini, ilifikishwa kwa kampuni itakayosafirisha kwenda Tanzania kwa mazishi," alisema Balozi Bwana.

Kwa mujibu wa Balozi Bwana, miili ya Watanzania hao itasafirishwa kwa awamu mbili. Leo itasafirisha miili miwili ya Said Mohames Kisarazo na Ibrahim Mohamed Kisarazo kwa ndege ya AIRLINK Flight itakayoondoka Afrika Kusini saa 4:00 usiku na kuwasili Tanzania kesho saa 8:30 usiku.

Alisema mwili wa Amiri utasafirishwa kesho saa 2:30 asubuhi kwa ndege hiyo ya AIRLINK Flight itakayoondoka Afrika Kusini na kuwasili Tanzania saa 7:40 mchana.

"Kwa muktadha huo, ubalozi unawaarifu kuwa heshima ya mwisho kwa dua kwa marehemu hao wote watatu itafanyika jumatano (leo), kuanzia saa 4:00 hadi 5:00 asubuhi katika Ofisi za Undertaker (Today`s Hope Funeral Services) zilizoko 50 Juta Street, Braamfontein mkabala na Audi Car Dealer.

"Kwa heshima kubwa, Ubalozi unazidi kutoa pole kwa familia na shukrani nyingi kwa Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Tanzania na Benki ya CRDB, Kitengo cha Diaspora na CRDB Insurance Company, kwa kuuwezesha ubalozi kufanikisha mipango yote ya kusafirishwa kwa marehemu hao.

Aidha, unazishukuru taasisi zote za Tanzania na Afrika Kusini zilizohusika katika katika kuwezesha utambuzi wa marehemu hao," alisema.

Watanzania hao walifariki dunia kwenye ajali ya moto uliozuka kwenye jengo la ghorofa na watu takribani 74 kufariki dunia jijini Johannesburg Septemba, mwaka jana.


airtel
A REASON TO **IMAGINE**

**MUONGOZO WA GHARAMA ZA AIRTEL KUANZIA JANUARI - MACHI 2024**

| LIPIA KADRI UNAVYOTUMIA: KODI IMEJUMUISHWA | | Bei (TSh) |
|---|---|---|
| MITANDAO YOTE | TSh / sek | 0.50 |
| NDANI YA MTANDAO | TSh / sek | 0.50 |
| INTANETI | TSh / Mb | 9.35 |
| SMS ZA NDANI YA NCHI | TSh / Sms | 8.00 |
| SMS ZA NJE YA NCHI | TSh / Sms | 215.00 |

**MITANDAO YOTE**

| Muda | Bei(TSh) | Mitandao Yote (Dak) | SMS |
|---|---|---|---|
| Saa 24 | 500 | 30 | 25 |
| Saa 48 | 1,000 | 150 | 25 |
| Siku 7 | 1,500 | 150 | 50 |
| Siku 7 | 2,500 | 300 | 50 |
| Siku 30 | 5,000 | 400 | 100 |
| Siku 30 | 10,000 | 1,200 | 100 |

**BANDO ZA SMS**

| Muda | Bei(TSh) | SMS |
|---|---|---|
| Saa 24 | 200 | 200 |
| Siku 7 | 500 | 1,000 |
| Siku 30 | 1,000 | 10,000 |

**BANDO ZA INTANETI**

| Muda | Bei (TSh) | (MB) |
|---|---|---|
| Saa 24 | 500 | 246 |
| Saa 24 | 1,000 | 492 |
| Siku 3 | 2,000 | 985 |
| Siku 7 | 2,000 | 950 |
| Siku 7 | 2,100 | 1,024 |
| Siku 7 | 3,000 | 1,480 |
| Siku 7 | 5,000 | 2,460 |
| Siku 30 | 10,000 | 4,920 |
| Siku 30 | 20,000 | 9,850 |
| Siku 30 | 30,000 | 14,780 |
| Siku 60 | 50,000 | 24,600 |
| Siku 60 | 100,000 | 49,200 |

**BANDO ZA AIRTEL - AIRTEL**

| Muda | Bei (TSh) | Ndani ya Mtandao (Dak) | Mitandao Yote (Dak) | SMS |
|---|---|---|---|---|
| Saa 24 | 500 | 90 | 10 | 25 |
| Saa 48 | 1,000 | 260 | 40 | 25 |
| Siku 7 | 1,500 | 260 | 40 | 50 |
| Siku 30 | 5,000 | 1,000 | 250 | 100 |

**COMBO (DAKIKA + MB)**

| Muda | Bei (TSh) | Mitandao Yote (Dak) | SMS | Intaneti(MB) |
|---|---|---|---|---|
| Saa 24 | 1,000 | 40 | 10 | 350 |
| Siku 7 | 2,000 | 55 | 10 | 800 |
| Siku 30 | 10,000 | 400 | 10 | 3,600 |
| Siku 30 | 20,000 | 500 | 10 | 8,192 |

**BILA KIKOMO**

**MUONGOZO WA GHARAMA ZA KIMATAIFA (KODI HAIJAJUMUISHWA)**

| Nchi | BAND | Bei(TSh/Sek) |
|---|---|---|
| China, Canada, India, USA | Band 1 | 8 |
| Malaysia, Japan, Lebanon, Ethiopia, Nigeria, Pakistan, Yemen, Sudan, Kenya Airtel, Kenya Other Network, United Arab Emirates | Band 3 | 10 |
| REST OF AFRICA, Denmark, Germany, Ireland, Netherlands, Norway, Spain, Sweden, Oman, Italy, Ghana | Band 5 | 14 |
| Zambia, Dem. Rep. of Congo, Zimbabwe, Burundi, Malawi | Band 6 | 25 |
| France, Rest of World, South Africa, United Kingdom | Band 7 | 13 |
| Central African Republic, Sao Tome & Principe, San Marino, Montenegro, Cuba, Martinique, East Timor, Nauru, Papua New Guinea, Solomon Islands, Vanuatu, Wallis & Fatuna, Cook Islands, Kiribati, Tuvalu, Micronesia, Maldives, South Sudan, Comoros, Gambia, Latvia, Somalia, Bulgaria, Lithuania, Moldova, Albania, Belarus, Congo, Guinea, Guinea Bissau, Seychelles, Sierra Leone, Senegal, Samoa, Tonga, Uzbekistan, Vanautu, Cameroon, Chad, Gabon, Madagascar, Belgium, Switzerland | Band 8 | 47 |
| Uganda , Uganda celtel, Rwanda | Band 11 | 15 |
| Satellite, Inmarsat, Premium Diego Garcia, Ascension Island, St.Helena, GreenLand Falkland Islands, Tokelau, Dem. Rep. Of Congo, Special numbers, Chile, Australia Territories, Niue Island, Upt, Norfolk Island, Chile | Band 12 | 233 |

| BANDO ZA KIMATAIFA | MUDA | BEI YA BANDO (TSH) | DAKIKA |
|---|---|---|---|
| INDIA | Saa 24 | 1,000 | 25 |
| CHINA, USA CANADA | Saa 24 | 1,000 | 10 |
| AFRIKA KUSINI | Saa 24 | 3,000 | 4 |
| MASHARIKI YA KATI (UAE,Saudi Arabia,Yemen,Lebanon,Pakistan & Qatar ) | Saa 24 | 2,500 | 5 |
| ULAYA | Saa 24 | 5,000 | 4 |
| AFRIKA MASHARIKI (Uganda Kenya & Rwanda), OMAN | Saa 24 | 2,500 | 3 |
| INDIA | Siku 7 | 5,000 | 100 |
| CHINA, USA CANADA | Siku 7 | 5,000 | 50 |
| AFRIKA KUSINI | Siku 7 | 6,000 | 7 |
| MALAWI, DRC | Siku 7 | 10,000 | 8 |
| ZAMBIA | Siku 7 | 10,000 | 7 |
| MASHARIKI YA KATI (UAE,Saudi Arabia,Yemen,Lebanon,Pakistan & Qatar ) | Siku 7 | 5,000 | 10 |
| UK, ITALY, GERMANY | Siku 7 | 10,000 | 8 |
| AFRIKA MASHARIKI (Uganda Kenya & Rwanda), OMAN | Siku 7 | 5,000 | 6 |
| INDIA | Siku 30 | 15,000 | 300 |
| CHINA, USA CANADA | Siku 30 | 15,000 | 150 |
| AFRIKA KUSINI | Siku 30 | 15,000 | 20 |
| MALAWI, DRC | Siku 30 | 20,000 | 15 |
| ZAMBIA | Siku 30 | 20,000 | 15 |
| MASHARIKI YA KATI (UAE,Saudi Arabia,Yemen,Lebanon,Pakistan & Qatar ) | Siku 30 | 15,000 | 30 |
| UK, ITALY, GERMANY | Siku 30 | 20,000 | 24 |
| AFRIKA MASHARIKI (Uganda Kenya & Rwanda), OMAN | Siku 30 | 15,000 | 18 |

**SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | Dakika za kupiga simu | Dakika za kupokea simu | MB |
|---|---|---|---|---|---|
| Eneo -1 | Siku 3 | 10,000 | 5 | 5 | 75 |
| Eneo -1 | Siku 7 | 25,000 | 15 | 10 | 250 |
| Eneo -1 | Siku 14 | 40,000 | 25 | 20 | 500 |
| Eneo -2 | Siku 3 | 25,000 | 12 | | 250 |
| Eneo -2 | Siku 7 | 50,000 | 15 | | 200 |

**SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | MB |
|---|---|---|---|
| Eneo -1 | Saa 24 | 5,000 | 500 |
| Eneo -1 | Siku 3 | 10,000 | 1,299 |
| Eneo -1 | Siku 7 | 15,000 | 2,048 |
| Eneo -1 | Siku 14 | 30,000 | 5,120 |

**SAFARI ROAMING BANDO - KUPIGA NA KUPOKEA SIMU**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | Dakika za kupiga simu | Dakika za kupokea simu |
|---|---|---|---|---|
| Eneo -2 | Siku 7 | 10,000 | 10 | |

**SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | MB |
|---|---|---|---|
| Eneo -3 | Siku 3 | 40,000 | 1024 |
| Eneo -3 | Siku 7 | 75,000 | 2048 |
| Eneo -3 | Siku 14 | 200,000 | 5120 |

**SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | MB |
|---|---|---|---|
| Eneo - 4 | Siku 3 | 35,000 | 200 |
| Eneo - 4 | Siku 7 | 90,000 | 512 |
| Eneo - 4 | Siku 14 | 175,000 | 1024 |

| | |
|---|---|
| **Eneo 1** | Kongo B(Airtel), DRC(Airtel), Gabon(Airtel), Ghana(Airtel),Kenya(Airtel), Madagasca(Airtel), Malawi(Airtel), Niger(Airtel), Nigeria(Airtel), Rwanda(Airtel), Seychelles(Airtel), Tchad(Airtel), Uganda(Airtel), Zambia(Airtel), India(Airtel) & Mauritius(Emtel) |
| **Eneo 2** | **AFRIKA:** Botswana(MTN), KongoB(Airtel), KongoDRC(Airtel), Egypt(Orange), Gabon(Airtel), Ghana(Airtel), Kenya(Airtel), Madagascar(Airtel), Malawi(Airtel), Mauritius(Emtel), Mozambique(Vodafone), Niger(Airtel), Nigeria(Airtel), Rwanda(Airtel), Afrika Kusini (MTN, Vodafone), Swaziland(MTN), Tchad(Airtel), Uganda(Airtel), Zambia(Airtel) |
| | **MAREKANI:** (T-Mobile) & CANADA: (Bell, Telus) |
| | **MASHARIKI YA KATI NA ASIA YA KATI:** China(China Mobile), Bangladesh(Airtel), India(Airtel), Israel(Pelephone, Cellcom), Oman(OmanTel), Pakistan(Telenor, Vimplecom), Qatar(Qtel), SaudiArabia(Zain), SriLanka(Airtel), Turkey(Vodafone), UAE (dU, Etisalat) |
| | **ULAYA:** Denmark(Telenor, TDC), France(Orange, SFR), Germany(T-Mobile, Vodafone), Greece(T-Mobile), Italy(Vodafone,Tim), Netherlands(Vodafone, KPN), Norway(Telenor), Romania(Vodafone, Orange), Russia(Vimpelcom), Spain(Vodafone, Telefonica), Sweden(Telenor), UK(Vodafone,Telefonica) |
| | **OCEANIA**: New Zealand(Vodafone) |
| **Eneo 3** | **AFRIKA:** Botswana(MTN), Cameroun(Orange), Egypt(Orange), Ghana(Airtel, TIGO), Ivory Coast(Moov), Mali(Orange), Mozambique(Vodacom), Mauritius(Emtel), Senegal (Orange), Swaziland(MTN), South Africa(MTN, Vodacom) |
| | **MAREKANI:** (T-Mobile) & CANADA: (Bell, Telus) |
| | **ULAYA:** Belgium(Base, Orange), Switzerland(Swisscom), Denmark(Telenor, TDC), France(Orange, SFR), Germany(T-Mobile, Vodafone), Greece(Cosmote), Ireland(Vodafone), Italy(Vodafone,Tim), Luxembourg(P&T), Netherlands(Vodafone, KPN), Norway(Telenor), Poland(T-Mobile), Romania(Vodafone, Orange), Russia(Vimpelcom), Spain(Vodafone, Telefonica), Sweden(Telenor), UK(Vodafone,Telefonica |
| | **MASHARIKI YA KATI NA ASIA YA KATI:** India(Airtel), Indonesia(Telkomsel), Israel(Orange, Jordan(Orange), Malaysia(Digi), Pelephone, Cellcom),Pakistan(Mobilink, Telenor), Qatar(Qtel), SaudiArabia(Zain), Sri Lanka(Airtel), Turkey(Vodafone), UAE(Etisalat) |
| | **CHINA:** China Mobile |
| **Eneo 4** | **AFRIKA: Afrika Kusini**(Cell C) |
| | **MAREKANI:** AT&T |
| | **MASHARIKI YA KATI NA ASIA YA KATI:** Oman (OmanTel), UAE (dU), Turkey (Turkcel) |

*Vigezo na masharti kuzingatiwa. Kwa maelezo zaidi tafadhali tembelea tovuti yetu: https://www.airtel.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hili la watumishi kuhamishia ofisi vituo vya mabasi halikubaliki

**ZIARA** zinazofanywa na viongozi ziwe za kichama au kiserikali zinasaidia kuibua mambo ambayo yamejificha na wananchi kushindwa pa kuyasemea.

Wakati Katibu wa Itikadi na Uenezi Taifa wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, alipokuwa kwenye ziara yake ya kichama mkoani Kilimanjaro, wilayani Same, ziliibuka kero kutoka kwa wananchi wakiwatuhumu baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa wilaya hiyo kwa kufungua tawi kienyeji la kusikiliza kero za wananchi ndani ya kituo cha mabasi.

Wananchi hao waliibua kero hiyo katika mkutano aliouitisha Makonda alioufanya katika Mji wa Same baada ya mmoja wa wakazi wa eneo hilo, kutoa masikitiko yake ya namna ofisi hiyo ya Mkuu wa wilaya, inavyoonekana na usumbufu wakati wa kuwasilisha malalamiko yao.

Imedaiwa kuwa baadhi ya watendaji wanachukua baadhi ya nyaraka wanazopeleka wananchi kwa ajili ya malalamiko na badala ya kuzishughulikia kwenye ofisi hiyo wanaitwa kwenye baa na maduka ili kujadili.

Hatua ya watumishi hao inashangaza na inaleta picha mbaya ya kujenga mazingira ya rushwa.

Vile vile, watumishi hao haileweki wana nia gani kuamua kufanya uamuzi huo kama sio kumharibia mkuu wao wa wilaya na yeye aonekane yuko pamoja nao.

Wananchi wanahoji hawajui lengo ni nini na wameomba waambiwe kama hayo ndio maeneo husika ya kusikilizia kero au wanatengeneza mazingira ya kumharibia mkuu wao.

Hata hivyo, wananchi wamekiri kuwa mkuu wao wa wilaya hana baya na wananchi wake isipokuwa anaangushwa na watendaji wake.

Wakati mwingine kiongozi unaweza kuona mambo hayaendi vizuri kwa kuamini watendaji wako wa chini kuwa wanatekeleza wajibu wao, kumbe hao ndio wanaokuharibia.

Kama Makonda asingetoa fursa ya kusikiliza kero za wananchi, hayo yote yasingejulikana kwa sababu hawakuwa na sehemu ya kusemea kero yao.

Na pengine walikuwa wakiona fursa ya kukutana na mkuu wao wa wilaya, lakini wanawekewa mizengwe ili njama yao isijulikane.

Pia, ni jambo zuri alililoagiza Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro la kila wilaya kuwa na dawati la malalamiko kwa ajili ya kupokea kero za aina mbalimbali na kwa Wilaya ya Same, imepangiwa kila Alhamisi.

Alikiri kuwa Ofisi ya Mkuu wa wilaya, hakuna watendaji wenye weledi wa kupokea kero za wananchi.

Mwananchi mmoja aliwalipua watumishi hao kwa kueleza kuwa wana tabia ya kuwaita wananchi wenye kero kwenda kituo kikuu cha mabasi Same kwa ajili ya kuwasikiliza.

"Katika hali isiyo ya kawaida, kiongozi kutoka ofisi ya mkuu wa wilaya anakuita stendi katika kibanda chake cha biashara ili akusikilize kwa jambo ambalo wewe ungelifikisha ofisi ya mkuu wa wilaya."

Kutokana na malalamiko hayo, wameitafsiri ofisi hiyo kugeuka kaa la moto hususani wanapokwenda kufuata haki zao.

Pia, licha ya kuwapo kwa dawati la malalamiko siku hiyo iliyopangwa bado suala la kuonana na mkuu wa wilaya hiyo ni changamoto.

Baada ya malalamiko hayo ya wananchi kiongozi huyo wa chama tawala alishangazwa na kitendo cha watendaji kuhamishia ofisi ya mkuu wa wilaya kituo kikuu cha mabasi na kwamba huo sio utaratibu.

Utaratibu uliowekwa na Serikali ofisi za umma ni kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali za wananchi na kuwaonya watendaji kuacha tabia ya kuichafua serikali kwa kutoa majibu machafu kwa wananchi.

Ziara hizi za viongozi ziwe za mara kwa mara na pia waliopewa majukumu ya kusimamia wananchi wasijifungie ofisini watoke kusikiliza kero zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Restuta James

# Mikutano, maandamano itakavyofyeka uchawa

**NI** siku 386 leo baada ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, aondoe marufuku ya mikutano ya hadhara na kuviruhusu vyama vya upinzani kukutana na wananchi katika majukwaa hayo.

Mwaka mmoja na siku 21 umetimia kwa nuru zaidi kuonekana baada Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kudai kuruhusiwa kufanya maandamano ya amani.

Maandamano hayo yanayolenga kuishinikiza serikali kufanyia kazi maoni ya wadau kuhusu upatikanaji wa katiba mpya na kuwapo chaguzi huru, haki na zinazokubalika.

Bila shaka, haya ni matunda ya zile R4 za Rais Samia ambazo ni maridhiano, ustahimilivu, mageuzi na ujenzi mpya.

Mambo muhimu yanayokumbushwa kwenye R4 ni tunu zetu ambazo ni utu, umoja, udugu, maelewano, ushirikiano, pamoja na amani.

Tunakumbuka jinsi ambavyo kampeni mbalimbali za vyama vya upinzani miaka saba iliyopita zilivyosaidia wabunge na madiwani wa vyama vyote kuwa macho na kuwatumikia wananchi kwa kiwango kikubwa.

Ni wazi kwamba mikutano na maandamano yatawezesha CCM na serikali kupata picha ya upande mwingine kuhusu kile ambacho wananchi wanakihitaji kutoka kwa viongozi wao na kuififisha 'tunu' yetu mpya ya 'uchawa'.

Nimekuwa nikijiuliza tumetoka kwenye utu na uzalendo kwenda kwenye uchawa, mwisho wetu utakuwa ni nini?

Nakumbuka kwamba kabla ya uchaguzi mkuu mwaka 2015, ilikuwa ni kawaida kukuta makada na mashabiki wa chama A wakiwa pamoja na wa chama B, hadi walipeana lifti wakiwa wamevalia mavazi ya vyama vyao. Baada ya kumalizika kwa uchaguzi na mikutano kupigwa marufuku, ukapandikizwa uadui mkubwa.

Hili ni jambo hatari kwa afya ya umoja na mshikamano wa nchi yetu.

Uchawa umeondoa ushirika, maelewano, uvumilivu na kujenga hasira kiasi cha aliye upande huu kutokuwa 'tayari' kusikiliza hata pale upande mmoja unapokuwa na hoja ya kuisaidia nchi.

Maandamano ambayo yapo dunia nzima na hata katiba yetu inayaruhusu, yanawapa fursa watu walio na imani moja katika jambo fulani kutoa hoja, elimu au hamasa ya jambo lenye manufaa ya wengi na ndio maana yapo maandamano ya kupinga mathalani ukatili wa kijinsia na kadhalika.

Ushauri wangu ni kwa wenye mamlaka katika ngazi mbalimbali, kujibu hoja kwa vitendo na kuuelimisha umma pale inapohitajika kuhusu kufanyiwa kazi kwa hoja kadhaa zilizoibuliwa.

Siyo dhambi kwa mfano kusema watoto wanakaa chini shuleni, hakuna vyoo, kuna mianya ya ubadhirifu wa fedha za umma na hoja hizo kujibiwa.

Wananchi hata kama ni wachache kiasi gani, wangependa kusikia kutoka kwa viongozi wao ni namna gani wanashughulikia changamoto zinazowakabili, kuliko mapambio ya 'chawa'.

Hata wakati wa kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi miaka ya 1990, pamoja na kwamba ripoti ya Jaji Francis Nyalali, ilionesha watu wengi kuuhofia, Mwalimu Julius Nyerere, alitaka maoni ya hao wachache walioutaka waheshimiwe.

Kuheshimu maoni ya wachache, ndio matunda ya zao la vyama vingi na kupanuka kwa wigo wa uhuru wa kutoa maoni miongoni mwa wananchi, kwa sababu isingekuwa rahisi sana mathalani kwa mwanachama wa CCM kupinga baadhi ya mambo yasiyomridhisha hadharani.

Akiwa nje ya chama hicho au serikali, inakuwa rahisi kuonesha ufa ili uzibwe na kwa kuwa unafanya hadharani, anaungwa mkono na wengine waliouona, tatizo linashughulikiwa kwa urahisi zaidi.

Kwa nchi iliyoamua kufuata mfumo wa kidemokrasia wa vyama vingi, mikutano na maandamano ni afya ya kuimarisha ili wenye mamlaka wasilale na asiwepo mtu wa kubweteka na kazi alizofanya. Hili ndilo linalonipa moyo kwamba rukhsa hii itaondoa uchawa ulioanza kuota mizizi nchini.

HABARI KITAIFA

## Serikali yajivunia kutengeneza ajira bunifu 4,000 kupitia UNDP

**Na Pilly Kigome**

AJIRA 4,000 kwa vijana zimetengenezwa katika kipindi cha mwaka 2023 kwa kupata utaalamu katika mpango ubunifu ya funguo uliotekelezwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na kushirikiana na Serikali ya Uingereza.

Jumla ya Sh. bil.4 zimetolewa katika kampuni 43 changa za kibunifu za vijana, ili kuwawezesha vijana msaada wa kitaalamu.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Dk. Tausi Kida alipokuwa akizungungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam katika mkutano wa kamati tendaji ya mradi wa Begin.

Dk. Kida alisema Umoja wa Ulaya EU umetoa jumla ya Sh.bil. 63.5 ambazo zimeelekezwa kufadhili miradi mitatu ikiwemo ya uboreshaji wa mazingira ya biashara(MKUMBI) ambapo awali ulikuwa ukijulikana kama BLUEPRINT.

Mradi wa pili ni ule wa QUALITAN uliojikita kuimarisha maabara za Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na tatu ni ule mradi wa FUNGUO ambao umejikita katika kuwezesha kampuni changa zinazochipukia.

Dk. Kida alifafanua katika utekelezaji wa miradi hiyo walifanikiwa kupitia mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (MKUMBI) imewezesha sekta binafsi kufanya kazi kiufanisi.

Kupitia utekelezaji wa mpango huo katika kipindi cha mwaka 2017/18 na 2022/23 serikali imepunguza na kuondoa zaidi ya tozo 374 na kurekebisha zaidi ya sheria na kanuni 55 katika sekta ya uwekezaji, kilimo, mifugo, uvuvi, malisasili, utalii, nishati, madini, viwanda na biashara. Matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kutoa huduma mbalimbali ikiwemo leseni, vibali na ada ikiwemo na uwepo wa kaguzi wa pamoja kwa taasisi za udhibiti, kupungua kwa idadi ya siku za kupata huduma kutokana na matumzi ya kieletroniki katika taasisi za umma katika kutoa huduma.

Pia uanzishwaji wa mfumo wa dirisha moja la huduma Tanzania Electronic Investment Window (Telw) ambao unamuwezesha mwekezaji kupata huduma mahali pamoja zikiwemo namba ya utambulisho wa utaifa, namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN), msamaha wa kodi, usajili wa kampuni, kibali cha kazi, hati ya ukaazi, haki ya umiliki na cheti cha uwekezaji.

Mwakilishi kutoka UNIDO, Dk.Victor Djemba alisema miradi hiyo imeweza kuleta matokeo chanya kwa kutoa mafunzo ndani ya nje ya nchi ya kuwajengea uwezo wa kitaalamu Shirika la ViwangoTanzania (TBS).

TBS sasa inaweza kuwasilisha maombi ya kutambukiwa kwa huduma zake bodi za kimataifa zinazosimamia viwango.

Mwakilishi kutoka UNDP, Dk. Shigeki Komatsuha, alitaja mafanikio ya miradi hiyo ikiwemo TBS imeweza kuendelea na mchakato wa manunuzi ya vifaa nya maabara na Tehama kutoa huduma za viwango na zenye ubora.

# Wilaya yajizatiti kukabili mafuriko

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

SERIKALI wilayani Morogoro imeandaa mipango ya muda mrefu na muda mfupi ikiwamo kujenga kuta kubwa mbili ili kunusuru mafuriko katika Shule ya msingi Juhudi iliyoko kata ya Lukobe.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Rebecca Nsemwa, alisema hayo jana kwenye taarifa yake iliyosomwa kwa niaba yake na Mjumbe wa Kamati ya Utatuzi Changamoto za Mafuriko kwenye shule hiyo, Winfred Kipako.

Alisema kutokana na mafuriko kuiandama shule hiyo na maji kuingia madarasani, wilaya imependekeza kuwekwa kuta hizo zitakazogawa maji kwenye mifereji hadi Mto Ngerengere.

"katika mipango ya muda mfupi kwa ajili ya kukabiliana na maji mengi yanayoingia shuleni hapa, tunapendekeza kujengwe kuta kubwa mbili upande wa nyuma na pembeni ya shule ambazo zitagawa maji kwa asilimia 50 kwa 50 kupeleka katika makorongo mawili ya maji maarufu ya eneo la Azimio na Lukobe ambayo hupeleka maji mto Ngerengerea' alisema Nsemwa.

Nsemwa alisema katika mipango ya muda mrefu, wilaya itaandaa utaratibu wa kujenga mabwawa makubwa mawili ya kuzuia wingi wa maji kwa kuyakusanya yakitokea maeneo ya Mkundi na Kilolo kabla hayajaingia kwenye milango ya njia za reli iliyojengwa na kampuni ya SGR na kuingia katika kata ya Lukobe na kuleta athari shuleni na kwenye nyumba na miundombinu mbalimbali ya barabarani.

Diwani wa Lukobe, Selestine Mbilinyi, alisema suala la mafuriko ni gumu ambalo linahitaji kupatiwa ufumbuzi wa haraka na kwamba mipango iliyoandaliwa na serikali ya wilaya ina uwezo wa kuiweka Lukobe katika amani kuliko ilivyo kwa sasa.

Alisema mvua inayoendelea kunyesha imesababisha athari katika kata hiyo hasa upande wa Shule ya Msingi Juhudi, kusababisha visima vya maji vinavyotegemewa kwa matumizi shuleni hapo kujaa mchanga na kufukiwa kabisa, hivyo kusababisha shule kukosa maji na kutishia afya za wanafunzi wanapokwenda vyooni.

Mbilinyi pia alisema mafuriko hayo yamesababisha athari upande wa miundombinu ikiwamo madaraja kumeguka na barabara nyingi kutopitika na kaya nyingi kujaa maji. Pia alisema baadhi ya kuta za nyumba na uzio vimeanguka na kusababisha taharuki kwa wakazi ha kata hiyo.

Mmoja wa wakazi wa kata ya Lukobe, Fatuma Zuberi, aliiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuwahamisha wakazi wa maeneo ya jirani na shule kwa kuwa imefikia wakati wanaogopa kulala kwenye nyumba zao na kukimbilia kwa majirani kwa hofu ya mafuriko.

Alisema wamekuwa wakikumbwa na mafuriko ya mara kwa mara hasa baada ya ujenzi wa reli ya SGR kukamilika ulioweka vizuizi na njia za maji kuelekezwa kwao kupita njia tofauti, na hivyo kusababisha madhara makubwa ikiwemo maji kujaa ndani ya nyumba na kuharibu mali mbalimbali.




Mkurugenzi Mtendaji wa CreditInfo Tanzania, Edwin Urasa (kushoto) na Mkurugenzi wa Kimataifa wa ICRA Rating Agency, Zeeshan Khan wakibadilishana makabrasha, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini mkataba wa kutoa huduma za tathmini ya mikopo kwa taasisi za fedha ili kutengeneza fursa mpya kwa mabenki na taasisi ndogo za fedha nchini ili kutambulika kimataifa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanza walia nakukithiri makali mgawo wa umeme

**Na Christina Mwakangale,**
MWANZA

WAKAZI wa Jiji la Mwanza, wamepaza sauti zao, hususan wafanyabiashara wa hoteli na sehemu za kutoa huduma za afya, kwa kulitaka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kutoa ratiba ya mgawo wa umeme inayoeleweka.

Pia wamesema biashara zinahitaji kutumia gharama kubwa katika uendeshaji, kutokana na kulazimika kutumia jenereta linalotumia mafuta ya dizeli ambayo inauzwa kwa Sh. 3,236 kwa lita.

Nipashe imefanya uchunguzi kwa siku tano kuanzia mwishoni mwa wiki, imebaini nishati ya umeme inakatika kila siku na ukiwapo unadumu chini ya saa sita hadi nane kwa siku, na kufanya baadhi ya wafanyabiashara zinazotumia umeme kufunga kwa muda.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, jijini Mwanza, mmiliki wa duka la samaki, Florence Masanja, alisema hifadhi samaki ni kwa saa 24 katika friji, ingawa sasa inamlazimu kununua mzigo kidogo ambao hautakaa muda mrefu.

"Awali kabla ya mgao huu kuanza tangu mwaka jana, samaki nilinunua moja kwa moja mwaloni (Ziwa Victoria), wasiopumgua Sh. 500,000 najua nikihifadhi kwenye friji hata wasipoisha kwa siku, kesho nitakuta hawajachina.

"Sasa nanunua kidogo tu kwamba nisifunge biashara, kwa sababu ndio tegemeo na familia yangu. Wateja nao wanaona waende moja kwa moja kununua samaki mwaloni huku katika maduka hawana uhakika," alisema. Mmoja wa wafanyabiashara wa hoteli jijini hapa ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, alisema amejiwekea ratiba ya kuwasha jenereta usiku tu na iwapo umeme umekatika mchana, huduma zinazotumia umeme husimama.

"Hebu fikiria umeme unakatwa saa 12 asubuhi na unarudi saa 12 jioni. Na ukifika hata saa 6 usiku unakatika, utarudi kwa saa chache na utakatwa tena alfajiri.

"Kimsingi ratiba haieleweki ni ya saa 12, nane au 18. Kwa ujumla umeme si wa uhakika na kuliwasha jenereta saa zote ni hasara. Lita moja ni zaidi ya Sh. 3,000 hivyo nimeweka ratiba bora niwashe jenereta usiku," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya Magu, Masele Luhende, aliiambia Nipashe kwamba, kwa siku wajawazito wanaofanyiwa upasuaji kwa siku ni takribani sita huku kwa mwezi ni 60 hadi 80.

"Kwa hali hii ya mgao wa umeme kwa mwezi inapaswa kutengwa Sh. mil 1.8 hadi mbili ni fedha za ndani. Na huwezi kuacha kuwa na umeme kwa sababu kuna upasuaji hasa kwa wanaojifungua. Kwa mwezi wanaojifungua ni 300 hapa Magu," alisema Dk. Luhende.

Nipashe imeshuhudia maduka makubwa ya biashara kama vile 'malls', mabenki, taasisi za binafsi na za umma, saluni, hospitali, hulazimika kutumia jenereta kwa zaidi ya saa 12, hadi jioni.

"Nimefika mwaka nikitokea Dar es Salaam, nimekaa kwa zaidi ya saa 18 bila umeme, haya ni mateso sana ni lazima serikali ichukue hatua madhubuti,"alisema.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Kisesa, Dk. Bijengo Mabiba, kuhusu suala la umeme alisema umeme hukatikakwa takribani saa 12 hadi 18 kwa siku, Hali inayofanya huduma za x-ray, upasuaji na uchunguzi kuwa duni.

"Umeme ni changamoto kuna baadhi ya vipimo huwa vinahitaji tu umeme tofauti na kipimo cha malaria ambacho hata bila umeme majibu hupatikana," alisema Dk. Mabiba.

"Tatizo ni kwa mama mjamzito ambaye anahitaji kufanyiwa upasuaji kwa dharura, inabidi tumpe rufani kwenda Sekou Toure, ambako ni kilomita 18 kutoka hapa (Kisesa), ili awahi huduma," aliongeza.

# Dola bilioni mbili kusafisha Ziwa Victoria

**Na Joseph Mwendapole**

KAMISHENI ya Bonde la Ziwa Victoria, inatarajia kutumia Dola za Marekani bilioni mbili kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kuweka mazingira safi ya ziwa hilo.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Miradi wa Kamisheni hiyo, Hilda Luoga, wakati akizungumza kwenye mkutano wa wadau wa nchi tano za Afrika Mashariki. Nchi hizo ni Tanzania, Kenya, Rwanda, Burundi na Uganda.

Alisema mradi huo utawezesha ajira nyingi za vijana watakaohusika kwenye shughuli mbalimbali na kwamba tayari kamisheni hiyo imeshafanya mazungumzo na nchi hizo tano za Afrika Mashariki na wameonyesha kuunga mkono kuanza kwa mradi huo.

"Kamisheni imeshakutana na Rais wa Benki ya Dunia (WB) anayeshughulikia Mashariki na Kusini mwa Afrika wakati wa kilele cha mkutano wa viongozi uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia na tulikubaliana kuhusu mradi huu," alisema.

Pia alisema wanaangalia maendeleo endelevu ya Ziwa Victoria kwa kuandaa mikakati ya miradi ya kutatua changamoto ya kukabili uchafuzi wa mazingira ya ziwa hilo kwa majitaka yanayotoka kwenye makazi ya watu na kwenye viwanda mbalimbali.

Alisema WB imekuwa ikifadhili Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi katika miradi ya kukabiliana na uchafuzi wa ziwa na mwaka 2020 ilifanya utafiti wakakuta kuna vyanzo vikuu vitatu kwenye ziwa hilo.

Ofisa huyo alisema WB ilibaini kuwa uchafuzi huo unatokana na vyanzo vikuu vitatu ambavyo ni majitaka kwenye makazi, kutoka kwenye viwanda na matumizi mabaya ya ardhi.

"WB iliona ni vyema kuliko kila nchi kuwa na mkakati wake sasa wote tuwe na mkakati endelevu wa pamoja wa wadau wote na kwa nchi zote ambao unaitwa Lake Wide Inclusive Sanitation na tangu hapo tumekuwa na mkakati uliohusisha wadau wa nchi zote kuondoa changamoto zilizopo," alisema.

Luoga alisema WB ilifanya utafiti na kubaini kwamba kuna miji mitatu ambayo ndiyo kiini cha uchafuzi wa mazingira kwenye Ziwa Victoria ambayo ni Mwanza, Entebbe Uganda na Homabay nchini Kenya.

"Baada ya kuibaini miji hii sasa wamekuja na mkakati maalum kwa miji hiyo na imetusaidia sana sisi kutafuta ufadhili wa kutekeleza mikakati hiyo na tumezungumza na WB tumewapa mapendekezo ya mradi mkubwa utakaoangalia utatuzi wa majitaka, takataka na mifereji inayopeleka maji ziwa Victoria," alisema



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege (wa pili kushoto), akikabidhi vifaa vya kilimo kwa vijana walio kwenye mpango wa 'Build a Better Tommorow' iliyopo chini ya Wizara ya Kilimo, katika halfa iliyofanyika Chinangali Dodoma jana. Benki hiyo, inafadhili vifaa na zana za kilimo zinazotumika kwenye programu hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tovuti ya Dk. Salim yatoa matukio ya kihistoria

**Na Elizabeth Zaya**

TOVUTI ya hifadhi ya nyaraka za Waziri Mkuu mstaafu, Dk. Salim Ahmed Salim, imetoa matoleo maalum mapya yenye nyaraka zinazoonyesha matukio mbalimbali ya kihistoria barani Afrika na duniani.

Matoleo hayo ni yale ambayo kiongozi huyo aliwahi kushiriki moja kwa moja.

Akizungumza kwa niaba ya familia, mtoto wa kiongozi huyo, Ahmed Salim, alisema wameamua kutoa matoleo hayo ikiwa ni sehemu ya kusherehekea miaka 82 ya kuzaliwa kwa baba yao.

"Dk. Salim Ahmed Salim, Waziri Mkuu mstaafu wa Tanzania na Katibu Mkuu mstaafu wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (sasa Umoja wa Afrika), anatimiza miaka 82 leo (jana). Kama sehemu ya kusherehekea umri wake mpya, Tovuti ya Hifadhi ya Nyaraka zake ya www.salimahmedsalim.com, imetoa matoleo mapya ya nyaraka yanayojumuisha matukio mbalimbali ya kihistoria barani Afrika na ulimwenguni," alisema Ahmed.

"Matoleo haya mapya, yanayojumuisha nakala za mawasiliano ya kimaandishi za Dk. Salim ambazo ni pamoja na Israeli na Palestina kuhusu mkutano baina ya kiongozi huyo mstaafu na aliyekuwa kiongozi Mkuu wa Chama cha Ukombozi wa Palestina (PLO), uliofanyika 1990 hoja kubwa ikiwa ni kuzungumzia wasiwasi wa PLO juu ya upanuzi wa Israel."

Alisema tukio lingine lililopo katika matoleo hayo ni la mkutano wa Geneva uliohusu Rhodesia ambayo kwa sasa ni Zimbabwe juu ya jitihada za Uingereza za kufikia mwafaka wa kupata sera ya uhuru nchini Zimbabwe na historia ya Marekani na barua ya aliyekuwa mwanaharakati wa haki za kiraia na mke wa hayati Martin Luther King kwenda kwa Dk. Salim mwaka 1979.

Mengine ni mkutano baina ya Tanzania na Libya ikionyesha nakala za mawasiliano ya kimaandishi za Waziri Mkuu huyo mstaafu wa Tanzania na aliyekuwa Rais wa Libya, Muammar Ghadaffi, Machi 13, 1990.

Ahmed alisema matoleo hayo mapya ni sehemu ya kazi wanayoifanya ya kuboresha maudhui ya tovuti itakayokuwa ikifanyika kila baada ya miezi mitatu.

"Tumaini letu ni kwamba nyaraka hizi, ambazo ni nyongeza ya zile zilizomo kwenye tovuti, zitaibua mijadala juu ya siasa za kiafrika na kimataifa, na umuhimu wa uhusiano na nchi mbalimbali katika nyakati zisizotabirika.

"Tovuti ya Dk. Salim ni kavazi la siasa za kimataifa na jukwaa la kipekee linaloonyesha nafasi muhimu iliyochezwa na viongozi na nchi za kiafrika katika jitihada za kuleta amani na utulivu duniani. Inaishamirisha Tovuti ya Hifadhi ya Nyaraka za Rais Nelson Mandela, ambalo ni kavazi lingine la kidigitali barani Afrika linaloweza kufikiwa na mtu yeyote," alisema.

# TCRA yaonya huduma mawasiliano bila leseni

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imetoa onyo kali kwa umma na kuwataka watoa huduma wazingatie kanuni ili kuzuia utoaji wa huduma za mawasiliano bila leseni ikiwemo usalama wa mitandao, huduma za mtandao na vituo vya data nchini.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, kwa umma hivi karibuni ilieleza kuwa kutoa huduma za mawasiliano bila leseni ni ukiukwaji wa kifungu cha 14 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010 (EPOCA), kinachokataza watu binafsi, taasisi au kampuni kutoa huduma hizo bila kupata leseni inayotakiwa kutoka TCRA.

Katika taarifa hiyo, TCRA ilisisitiza umuhimu wa kuzingatia miongozo na sheria za udhibiti, huku ikiwatahadharisha Watanzania dhidi ya kutumia huduma za mawasiliano kama vile huduma za usalama mtandaoni, internet na vifaa vya kuhifadhia data vinavyotolewa bila ya leseni.

Aidha, Dk. Bakari alionya kuwa mamlaka itachukua hatua za kisheria dhidi ya mtu, taasisi au kampuni yoyote itakayobainika kukiuka kanuni kwa kutoa huduma za mawasiliano bila leseni.

Aliwahimiza wananchi kuimarisha mazingira ya mawasiliano yaliyodhibitiwa na halali kwa kuacha kujihusisha na watoa huduma wasio na leseni.

"Hii siyo tu kwamba inahakikisha usalama wa watu binafsi lakini pia inasaidia dhamira kuu ya TCRA ya kudumisha viwango vya juu zaidi vya huduma za mawasiliano nchini. TCRA itaendelea kusimamia ufuasi katika sekta ya mawasiliano na hatua zitachukuliwa dhidi ya mtu au kampuni itakayopatikana ikitoa huduma bila leseni katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisisitiza Bakari.

Mdau wa mawasiliano jijini Dar es Salaam aliyejitambulisha kwa jina la Joel Mwanakatwe, aliunga mkono msimamo wa TCRA, akisema kuwa hatua hiyo inaashiria nia ya mdhibiti kulinda maslahi ya umma.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010, mdhibiti wa sekta ya mawasiliano amepewa mamlaka ya kutoa, kupanua na kurejesha leseni za mawasiliano pamoja na kutekeleza masharti ya leseni dhidi ya watoa huduma na kumtia hatiani yeyote anayetoa huduma za mawasiliano bila kupata leseni halali.



## Sendiga kuwashughulikia makandarasi wasiolipa stahiki

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, ameapa kula sahani moja na makandarasi waliopewa zabuni za ujenzi wa miundombinu ya barabara na hawataki kulipa stahiki za wafanyakazi wao.

Sendiga, amesema hataki kuwaona makandarasi wa aina hiyo na kama akipelekewa malalamiko kuhusu jambo hilo, atawafukuza katika mkoa huo.

Alikuwa akizungumza jana wilayani humo na makandarasi hao pamoja na Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), wakati wa hafla ya utiaji saini mikataba saba yenye thamani ya Sh. bilioni 2.3.

"Ninyi mliotia saini leo (jana) mikataba hii, hakikisheni mnawalipa stahiki zao wafanyakazi wenu na kutoa ajira kwa wazawa, la sivyo nitawavuruga.

Alisema ni vizuri wakandarasi waliopewa kazi walinde kazi zao kwa kuwa na nidhamu na utendaji wao uwe mzuri.

"Wakandarasi ambao hawalipi stahiki za wafanyakazi wao siwataki na ninahitaji wakandarasi ambao wana uwezo wa kuwalipa watumishi wake," alisema Sendiga.

Awali, Meneja wa TARURA, Mkoa wa Manyara, Salimu Bwaya, alisema mikataba hiyo ni ya awamu ya pili, awamu ya kwanza ilikuwa mikataba 44.

Bwaya, alisema mikataba hiyo itasaidia kuboresha maeneo korofi na madaraja katika wilaya zote za mkoa huo.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Lema Investment Limited, Godwin Lema, aliahidi watafanya kazi kwa uaminifu.



# Vituo kudhibiti wanyamapori vyajengwa wilayani Mwanga

**Na Mary Mosha,** MWANGA

SERIKALI imeanza kujenga vituo vipya vya askari wa wanyamapori katika Wilaya za Same na Mwanga, mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu wa mazao, hasa tembo.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, alisema pia imeanza kujenga mabwawa ya maji, kwa ajili ya wanyama hao katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na maeneo mengine ya misitu katika wilaya hizo ili kuzuia wanyama hao wasiende katika makazi ya wananchi kutafuta maji na malisho.

Kairuki, alisema maendeleo ya mradi huo, baada ya kutakiwa kufanya hivyo na Katibu wa Itikadi na Uenezi Taifa wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda.

"Mbali na mradi huu kuanza, wizara imepanga kutumia ndege ndogo maalumu kwa ajili ya kuwafukuza tembo, watakapoonekana kukaribia makazi ya wananchi," alisema.

Kairuki alikuwa akijibu hoja za wananchi wa wilaya za Same na Mwanga, waliodai ndugu zao kupoteza maisha, kutokana na kuuawa na wanyama hao.

"Pamoja na vituo hivyo, tunatoa mafunzo kwa wananchi kupitia TAWIRI (Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania) na TAWA (Mamlaka ya Usimamizi na Uhifadhi wa Wanyamapori), namna sahihi ya kuishi na tembo, lakini kuwaepuka kuwachokoza, kwa sababu mnyama huyo ameonekana kuwa na kumbukumbu na kulipiza kisasi pale anapochokozwa," alisema.

Waziri alisema kwa wananchi wa Wilaya ya Same, wanadai zaidi ya Sh. milioni 240 za fidia ya kifuta jasho kutokana na kudhuriwa na tembo.

Katika mkutano wake wa hadhara uliofanyika Wilaya ya Same, Makonda aliitaka serikali kuharakisha malipo hayo kwa wananchi wanaodai fidia zao ili wanufaike na serikali.



Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Kheri James (kushoto) akimsikiliza Meneja wa Wakala wa barabara Tanzania (Tanroads) mkoani Manyara, Dutu Masele wakati wa ukaguzi wa barabara ya lami ya kilometa 25 ya Mbulu Garbabi ya gharama ya sh. bilioni 36, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wananchi wawachongea watumishi ofisi ya DC kwa Makonda

**Na Mary Mosha,** SAME

WANANCHI wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, wamewachongea watumishi wa ofisi ya Mkuu wa wilaya hiyo kwa Katibu wa Itikadi na Uenezi Taifa wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, kwa kufungua tawi kienyeji la kusikiliza kero za wananchi ndani ya kituo cha mabasi.

Jana, katika mkutano wa Makonda alioufanya katika Mji wa Same, mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Rehema Mshana, alitoa masikitiko yake ya namna ofisi hiyo ya Mkuu wa wilaya, inavyoonekana na usumbufu wakati wa kuwasilisha malalamiko yao.

"Mheshimiwa Makonda, baadhi ya watendaji wanachukua baadhi ya nyaraka tunazopeleka kwa ajili ya malalamiko na kutuita kwenye baa na maduka yaliyopo hapa Same Mjini ili kujadili.

"Hatujui lengo ni nini. Tunaomba tuambiwe kama ndio maeneo husika ya kusikilizia kero au wanatengeneza mazingira ya kuomba rushwa," alilalamika Rehema.

Aidha, alikiri mbele ya Makonda kwamba Mkuu wa wilaya hiyo, Kasilda Mgeni hana baya ila anaangushwa na watendaji wake.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, aliagiza kila wilaya kuwa na dawati la malalamiko kwa ajili ya kupokea kero za aina mbalimbali na kwa Wilaya ya Same, siku iliyotengwa ni Alhamisi.

"Ofisi ya Mkuu wa wilaya, hakuna watendaji wenye weledi wa kupokea kero za wananchi," alisema.

Rehema, alisema baadhi ya watendaji wa ofisi ya wilaya hiyo wamekuwa na tabia ya kuwaita wananchi wenye kero kwenda kituo kikuu cha mabasi same kwa ajili ya kuwasikiliza.

"Katika hali isiyo ya kawaida, kiongozi kutoka ofisi ya mkuu wa wilaya anakuita stendi katika kibanda chake cha biashara ili akusikilize kwa jambo ambalo wewe ulilifikisha ofisi ya mkuu wa wilaya."

Alisema wananchi wameitafsiri ofisi hiyo imegeuka kaa la moto hususani wanapokwenda kufuata haki zao.


Alisema licha ya kuwapo kwa dawati la malalamiko siku hiyo iliyopangwa bado suala la kuonana na mkuu wa wilaya hiyo ni changamoto.

Akijibu malalamiko ya wananchi, Makonda alishangazwa na kitendo cha watendaji kuhamishia ofisi ya mkuu wa wilaya kituo kikuu cha mabasi na kwamba huo sio utaratibu.

"Serikali imeweka ofisi za umma kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali za wananchi, wewe Mkuu wa wilaya tazama watendaji wako, watakuharibia," alionya.

Pia aliwataka watendaji wa serikali kuacha tabia ya kuichafua serikali kwa kutoa majibu machafu kwa wananchi.

Alisema CCM haitavumilia kuona baadhi ya watendaji wa serikali wanaochonganisha chama na serikali na kuahidi kuwa watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.





# Polisi yakamata watu 10 tuhuma mauaji ya mlinzi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza, linawashikilia watu 10 kutoka katika maeneo mbalimbali mkoani hapa kwa tuhuma za kuvamia, kupora vitu dukani na kumuua mlinzi wa duka hilo, Yumen Elias (54).

Juzi Nipashe iliripoti tukio la kuuawa kwa mlinzi huyo mkazi wa Nyanshishi, jijini hapa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali katika maeneo ya kichwani na watu hao wanaotajwa kuwa wezi kuiba vitu mbalimbali vya dukani humo.

Akithibitisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbroad Mutafungwa alisema, baada jeshi hilo kupata taarifa msako mkali ulianza kuwakamata watuhumiwa 10 waliohusika katika mauaji hayo.

Alitaja watuhumiwa hao kuwa ni Julius Joseph (22), Paul John (23), Leonidas Juma (19), Abdallah Hassan (31) na Edward Boniface (19).

Wengine ni Mussa Robert (22), Steven Emmanuel (18), George Mang'era (50), Hamis Omary (21) na Charles Chacha (27).

Kamanda Mutafungwa alisema jeshi hilo linaendelea kukamilisha upelelezi wa tukio hilo na utakapokamilika watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

Alizitaka kampuni za ulinzi mkoani hapa kuhakikisha kila lindo linaweka walinzi zaidi ya mmoja ili kusaidiana katika kazi hiyo na kuacha kuweka mlinzi mmoja ambaye uwezo wa kumudu watu wengi ni mdogo kwake pia aliziagiza kampuni hizo kuhakikisha kila mlinzi anapatiwa silaha pindi anapopewa lindo kwa ajili ya usalama wake pamoja na mali anayoilinda.

**Alitaja watuhumiwa hao kuwa ni Julius Joseph (22), Paul John (23), Leonidas Juma (19), Abdallah Hassan (31) na Edward Boniface (19).**



Maofisa Afya Kata ya Pamba na Jiji kutoka mkoani Mwanza, jana wakitoa elimu juu ya mlipuko wa ugonjwa wa Kipindupindu kwa mpika vitumbua anayetajwa kukiuka kanuni za afya kwa kuendelea kupika katika maeneo ya barabani ambayo ni hatarishi, mpaka sasa visa vya ugonjwa huo vimefikia 112 mkoani hapa. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Wananchi wachanga kujenga mitaro ya barabara

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Kata ya Majengo, Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamelazimika kujichangisha fedha kwa ajili ya kujenga mitaro katika barabara ili kuruhusu maji kufuata mwelekeo wake kukabiliana na mafuriko hususani katika kipindi hiki cha mvua.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Majengo, Shida Ally, alisema wamefikia hatua hiyo kutokana na mitaro katika barabara hiyo kukatika kutokana na mvua na maji kuingia katika makazi ya watu.

Alisema bado wanaendelea na michango ili mitaro hiyo ijengwe kwa ubora na tatizo hilo lisijirudie tena kwa kuwa mvua inaendelea kunyesha ni vyema kuchukua tahadhari mapema.

Kadhalika alisema katika michango hiyo wamepokea pia kutoka kwa Mbunge wa Jimbo Kahama, Jumanne Kishimba wa Sh. milioni 1.5 kutoka katika mfuko wa jimbo na ujenzi unaoendelea chini ya usimamizi wa serikali za mitaa pamoja na TARURA.

Alisema, kata za Majengo, Mhongolo, Mhungula, Nyihogo na Zongomela zipo chini na maji ya mvua yanakosa sehemu ya kupita na kuingia kwenye makazi yao na kusababisha uharibifu wa mali.

Mbunge Kishimba, alisema awali aliwapatia Sh. milioni 1.5 ambazo zimetumika kuchimba mitaro na mifuko 50 ya saruji ya Sh. milioni 1.2 na mawe ya ujenzi tripu 50 zenye thamani ya Sh. milioni 4.5.

"Wananchi wa kata za Nyihogo na Mhungulu tumewapatia fedha Sh. 500,000 kwa ajili ya kufanya usafi wa kuzibua mitaro ya maji barabarani, tumebaini mafuriko yanatokea kwasababu mitaro imeziba na kushindwa kupitisha maji inavyotakiwa," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wenyeviti wa serikali za mitaa kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) kuwahamasisha wananchi kufanya usafi mara kwa mara hususani wale waliopo kando ya barabara na kuacha tabia ya kutupa taka kwenye mitaro zinazosababisha maji kushindwa kupita.

## Mbaroni madai kumuua mdogo wake kwa sululu

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

ASTERIA Renatus (34), mkazi wa kitongoji cha Mwajuli, Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza anadaiwa kumuua mdogowake Mlingwa Renatus (15), mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Mwampulu kwa kumchoma kitu chenye ncha kali 'sululu' wakati wakiwa nyumbani.

Kwa mujibu wa wanafamilia, tukio hilo lilitokea juzi, Januari 21, wakati wazazi wao pamoja na watoto wengine wakiwa shambani na kumuacha Asteria nyumbani akiwa na mdogo wake.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbroad Mutafungwa, alisema mwanafunzi Renatus alifikwa na umauti akiendelea na matibabu katika Hospitali ya Sumve iliyoko wilayani humo.

Aidha, Mtafungwa alisema jeshi hilo linamshikilia mtuhumiwa huyo na anaendelea kuhojiwa ikiwa ni pamoja na kujua utimamu wa akili yake na atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Katika hatua nyingine Kamanda Mutafungwa aliviambia vymbo vya habari kuwa jeshi hilo limewakamata watu sita kwa tuhuma za kughushi nyaraka mbalimbali za serikali kwa lengo la kujipatia fedha katika matukio mawili kwa nyakati tofauti yaliyotokea Wilaya ya Nyamagana na Ilemela.

Alisema operesheni iliyofanyika Januari 15 hadi 19, mwaka huu katika wilaya hizo kwa kushirikiana na taasisi nyingine za serikali waliwakamata wakiwa na vielelezo mbalimbali ambavyo wamekuwa wakivitumia kughushi nyaraka hizo.

Waliokamatwa katika msako huo ni Vedastus Faustine (54), Joseph Katanga (47), Lameck Bilikwija (29), Paul Odumbe (58), Evarist Leonard (28) na Abdul Kiraka (29).

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu ili ziweze kufanyiwa kazi kwa haraka na pia litaendelea kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya wahalifu wote.



Ukurasa 12

## Adui wa haki rushwa adhibitiwe, ni hasara kuzidi kupambana naye



Ukurasa 13

## Ilivyo 'kisa na mkasa' Rais Samia kuwapasha viongozi CCM Visiwani


# siasa

JUMATANO JANUARI 24, 2024

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 14

## Mdudu anapoitafuna, kutishia kuimega EAC

# Ziara Makonda mikoani kama mahakama, ni misururu ya kesi

- Kali ni mmoja kupora mali kwa jina la chama

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa Tanga**

VIONGOZI wa CCM kushitakiwa kudhulumu, wananchi kuwakataa watendaji na migogoro mingi ya ardhi ni miongoni mwa misururu ya malalamiko yanayomkaribisha Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, mikoani.

Katika ziara yake ya mikoa 18, ikiwamo Pwani, Tanga na Kilimanjaro, anakutana pia na kilio cha kukosekana huduma bora za afya huku wananchi wakichangia fedha za ujenzi wa hospitali lakini viongozi wa halmashauri wakikaa kimya.

Akianzisha ziara yake Januari 19 mwaka huu mkoa wa Pwani kuelekea Tanga na kufikia mikoa mingine 18 ili kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi na kutatua kero za wananchi, anapokea malalamiko ya ardhi mkoani Pwani.

Akiwa Bagamoyo mkoani humo, wananchi wengi wanalalamikia changamoto ya migogoro ya ardhi, Makonda akiwataka watendaji wa serikali kufungua ofisi siku za mapumziko kusikiliza kero hizo na kuzitatua badala ya wananchi kuendelea kupata maumivu.

Anawataka kutatua kero za wananchi kwa kuwa uhai wa chama unategemea wananchi kwa sababu wamewapa ridhaa ya kuongoza nchi.

Makonda anashangazwa na madai ya kigogo wa CCM kupora nyumba, tatizo analokutana nalo Tanga, akisema amepatiwa taarifa za mwana CCM kuporwa nyumba yake na kiongozi wa chama huku, akionya kuwa huo si ubinadamu.

Akiibua tukio hilo, mmiliki wa nyumba, Nassor Fereji, anasema nyumba yake aliombwa na Mwenyekiti wa chama Wilaya ya Tanga Mjini, Meja mstaafu Khamis Mkoba, kwa sababu ipo jirani na ofisi ya CCM, akielezwa kuwa uongozi unataka kuweka makatibu na akakubali.

" Mimi ni mwana CCM, nikasema sawa hakuna shida makatibu ni wetu nikatoa nyumba yenye hati ya miaka 21 ambayo alikuwa nayo mmiliki wa kwanza nikauziwa nimekaa nayo miaka 11 mpaka leo hii ofa yangu inaonyesha ni miaka 33," anasema."

"Mwaka jana nikaona wanaanza ujenzi katika banda la uwani nikamfuata Mwenyekiti nikamuuliza ni vipi akanijibu hii yetu bwana sio yako tena nikamwambia inakuwaje mimi kuninyang'anya nyumba mwanachama nikamwambia hiki sio chama ni wewe. CCM haiwezi kufanya hivi, "anaongeza.

Fereji anasema ilibidi aende ardhi kuhakiki hati yake kujua kama iliibiwa au la akajulishwa namba 62 ni nyumba yake akatakiwa kuonyesha ofa yake na kueleza tatizo.

Makonda anamuagiza kiongozi huyo wa CCM kuirejesha nyumba hiyo mara moja kwa Fereji na kitendo alichokifanya sio tabia ya CCM bali mwenendo wake binafsi.

Anaendelea kusikiliza kero za wananchi wa Tanga Mjini na kupokea migogoro mingi ya ardhi na kuwataka viongozi hao kufungua ofisi Jumapili asubuhi kwa ajili ya kutatua kero hizo kwa kuwa wameshindwa kuzimaliza.

Makonda alifika katika ofisi hiyo asubuhi na kuwataka viongozi wajipange kila idara kwa ajili ya kuwasikiliza wananchi kwa kuwa wameshindwa kutekeleza majukumu yao siku za kazi, hivyo itawalazimu kuyafanyia kazi Jumapili.

Anasema migogoro mingi ya ardhi anayokutana nayo ni kutowajibika kwa watendaji na kama wangewajibika ipasavyo asingepokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi akiwaambia waache 'kuchati' ofisini.



Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, akizungumza na wananchi. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

**MKURUGENZI AMKERA**

Aidha, Makonda akiwa Wilaya ya Pangani anachukizwa na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Pangani, Isaya Mbenje, kushindwa kujenga zahanati kwa muda mrefu licha ya wananchi kuchanga fedha na nguvu.

Makonda anasema wananchi hao hawakutakiwa kujichangisha kujenga zahanati hiyo kwa kuwa wanalipa kodi, hivyo ni jukumu la serikali kujenga kwa sababu wananchi wanatembea kilometa saba kutafuta huduma ya afya jambo ambalo linahatarisha usalama wao.

**INAENDELEA UK. 12**

# Adui wa haki rushwa adhibitiwe, ni hasara kuzidi kupambana naye

**Na Dk Reubeni Lumbagala**

RUSHWA ina majina mengi utasikia mlungula, kitu kidogo, hongo, chai, chauchau na wapo wanaosema kunjua mkono, laini mchakato na hata zunguka mbuyu.

Kwa ujumla tafsiri ya neno 'rushwa' haibadiliki ni ile ile kutoa fedha au kitu kingine cha thamani hata mwili wa mwanamke ili kupata upendeleo au haki unayoitaka.

Rushwa pia ina maana ya matumizi mabaya ya ofisi kwa maslahi binafsi ambayo leo hali hiyo imekuwa tatizo la kijamii na duniani ambako kila nchi inafanya jitihada zake katika kuipunguza au kuikomesha .

Tanzania si kisiwa, hivyo rushwa inaikabili pia nchi hii na ndiyo maana juhudi mbalimbali zinafanyika kuipunguza au kuimaliza, zikianzishwa taasisi za kuikabili mfano ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ya Usuluhishi wa Malalamiko ya Kodi (TOST), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG).

Ipo methali isemayo "usipoziba ufa utajenga ukuta,"ikihimiza kurekebisha na kuondoa kasoro au jambo tangu linapobainika badala ya kuliacha tatizo kukomaa au kuwa kubwa huku madhara yake yakiwa na athari zaidi.

Aidha, ni methali inamaanisha pia kuacha kudharau jambo dogo, kwani linaweza kuongezeka na kuwa zito au usipozuia mambo madogo yatakuwa makubwa yanayoshindikana baadaye.

Kutokana na uwepo wa rushwa katika maeneo mbalimbali kama vile mahakamani, hospitalini, ofisini, shuleni, vyuoni na ndani ya jamii, ni muhimu kuweka jitihada kubwa katika kuzuia kuliko kupambana kwani gharama za mapambano ni kubwa kuliko za kuzuia.

Vita ya rushwa ni jukumu la kila mwananchi na si serikali peke yake. Ndiyo maana ni muhimu kuunganisha nguvu ya pamoja na taasisi zake kama TAKUKURU, asasi za kiraia na wananchi, ili kupiga hatua kubwa katika vita ya rushwa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene. **PICHA: MTANDAO**

> "Ni muda mwafaka sasa kuhakikisha kuwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kanuni na sheria zote zinazingatiwa ili kuondoa mianya ya rushwa.

Desemba 4, 2023, akiwa kwenye kongamano la jukwaa la kitaifa la wadau dhidi ya rushwa ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya maadili na haki za binadamu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, anazitaka taasisi zinazohusika kusimamia utawala bora kuzuia zaidi rushwa badala ya kupambana nayo.

Simbachawene anakemea hali iliyopo sasa ya kupambana na rushwa kwenye miradi ya maendeleo badala ya kuzuia ubadhirifu na hujuma zisitokee ili kupata thamani ya fedha kwenye miradi hiyo na kuleta tija kwenye maisha ya wananchi.

"Wakati mwingine tunaweka nguvu kubwa na raslimali nyingi katika kupambana na rushwa wakati ambapo matokeo ya rushwa yanakuwa tayari yameshatokea na kuleta madhara kwa serikali badala yake tulipaswa kutumia nguvu hiyo hiyo katika kuizuia, " anasema Waziri.

Halikadhalika, Simbachawene anarejea kwenye tafiti mbalimbali zilizofanywa nchini kuhusu hali ya utawala bora na kwamba zimebaini kuwa rushwa ni moja ya changamoto katika ufikiwaji wa lengo la serikali la kuleta maendeleo.

Wananchi wanakwama kupata maendeleo katika sekta kama vile maji, afya, elimu na miundombinu. "

Kutokana na tafiti kuonyesha rushwa inaathiri ufikiwaji wa maendeleo ya wananchi, hivyo basi ni muhimu kuzuia rushwa ili kuepuka kadhia hii ambayo inaathiri maisha ya wananchi kutokana na miradi kutekelezwa chini ya kiwango.

Halikadhalika wananchi kukosa kabisa miradi ya maendeleo ambayo kama ingetekelezwa ipasavyo, ingeweza kuboresha hali za maisha yao na kuchochea maendeleo na ustawi wa wananchi mijini na vijijini.

Ni muda mwafaka sasa kuhakikisha kuwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kanuni na sheria zote zinazingatiwa ili kuondoa mianya ya rushwa.

Mathalani, upatikanaji wa mzabuni wa kutekeleza miradi ya maendelo, apatikane kwa uwazi na akidhi vigezo vyote. Vilevile, hata baada ya kushinda zabuni hiyo, afuate sheria, taratibu na mifumo ya manunuzi kikamilifu katika kutekeleza mradi ili kazi ziakisi thamani ya fedha na wananchi wafurahie ujenzi au jambo linalofanyika.

Kama watendaji hawataziba nyufa kwa kutenda haki kwa wazabuni wanaotekeleza miradi ya maendeleo na kufuatilia ubora wa kazi, ni dhahiri watapatikana wasiokidhi vigezo na hivyo kufanyakazi chini ya viwango na itakuwa ni upotevu wa fedha za umma na kuwakosesha wananchi maendeleo.

Ni lazima ieleweke kuwa gharama ya kuzuia rushwa ni ndogo kuliko ya kupambana nayo. Uchaguzi ni wa serikali na Watanzania, kutumia fedha kidogo kuzuia au kutumia gharama kubwa katika mapambano.

Nchi bado ni maskini, bila kuzuia rushwa, wananchi wa chini au maskini ambao ni wengi wataendelea kupata shida kupata haki zao. Kila mwananchi awe wa kipato cha juu, kati au chini anapaswa afurahie kuishi Tanzania kwa kupata haki bila rushwa. Ikumbukwe usipoziba ufa utajenga ukuta, taifa lisifike huko kwenye mapambano ya rushwa taifa linalo nafasi ya kuziba nyufa sasa ili kuokoa mabilioni.

***Dk. Reubeni Lumbagala ni Mwalimu Mlali Sekondari, Kongwa-Dodoma. Maoni: 0620 800462.***

## Ziara Makonda mikoani kama, mahakama ni misururu ya kesi

**INATOKA UK. 11**

Akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Muheza anawajulisha amekuta kero nyingi zinazosababishwa na mkurugenzi na kwamba akiwa njiani amempigia simu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), akamjulisha mapendekezo ya CCM kuwa mkurugenzi Isaya Mbenje, asimamishwe kazi.

Anamuomba Waziri wa TAMISEMI Mohamed Mchengerwa kuunda timu ya kuchunguza iwapo baadhi ya wafanyabiashara wanawauzia halmashauri hiyo vifaa vya ujenzi wa zahanati hawalipwi na wakienda kwa mkurugenzi hawalipwi pia.

Makonda anasema ipo miradi mingi inakwamishwa kutokana na watendaji wa serikali ambao baadhi yao wanajiona ni miungu watu huku wananchi wakiendelea kuteseka.

Anawaagiza wenyeviti wa CCM katika wilaya kote nchini kutoa ripoti za wakuu wa wilaya na wakurugenzi wazembe kwenye maeneo yao.

Anawaambia Chama Cha Mapinduzi kitawatambua kwa majina watendaji wote wa serikali wazembe, wababaishaji na wanaowanyanyasa wananchi ili wachukuliwe hatua.

"Upande mmoja wapo wanaofanya vizuri lazima watambulike na waheshimike, upande wa pili wanaofanya vibaya lazima wachukuliwe hatua ili mwisho chama kishike hatamu," anasema Makonda.

### 'BRUFKESI' ZA NOTI

Viongozi wanaosubiri kugawa kanga na posho kukiona, ni onyo la Makonda akisema chama kitawashughulikia wasiofanya shughuli za kimaendeleo kwa wananchi na badala yake wamekaa wakisubiri kutoa posho na kanga kwa wajumbe ili wapate kura.

"Hatutaki wagombea siku za mwisho wanakuja na 'brufkesi' kugawa hela, wananunua kamati za siasa, wajumbe halafu tunapoteza uhalali hili hatuwezi kulikubali,"anasema Makonda.

### MATHAYO AKATALIWA

Mbele ya Mwenezi Makonda, wapigakura wa jimbo la Same Magharibi, wakamkataa mbunge wao, David Mathayo, kwa madai kuwa hatoi msaada kwa wananchi .

Wanadai wamemchoka kwa kuwa haonekani jimboni na bungeni hali inayokwamisha maendeleo yao huku wakimtaka asijaribu kugombea nafasi hiyo kwa kuwa hakuna alichokifanya.

Makonda anasema kipimo cha CCM kumpitisha kiongozi ni namna anavyowasaidia wananchi kuleta maendeleo katika maeneo wanayoyaongoza na si vinginevyo.

# Ilivyo 'kisa na mkasa' Rais Samia kuwapasha viongozi CCM Visiwani

• Awakumbusha kukubalika ndani ya soko la siasa

Na Peter Orwa



Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan, anapowatangazia Watanzania mwanzo wa vita dhidi ya rushwa na uzembe wakati wa uchaguzi. **PICHA: MTANDAO**

Ni wastani wiki moja sasa, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ametoa kauli nzito akiwa Zanzibar, chini ya kilemba chake Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi (CCM), dhidi ya viongozi 'wanaosuasua' wakitumika kiserikali kupitia karata ya chama hicho

Anawaonya wabunge na wawakilishi wasiotekeleza wajibu wao kuwa 'watakutana katika Uchaguzi Mkuu Ujao', salamu ambazo pia zinawafikia wanaojitosa katika nafasi za serikali za mitaa, kwamba 'wataonana' wakati mwafaka ukifika.

Umma umeshtuka kudadisi tafsiri ya kina kutoka kauli hiyo. Alikuwa katika ziara ya kichama baada tu ya kikao cha CCM kilichompata Katibu Mkuu mpya, Dk. Emmanuel Nchimbi, kuziba nafasi iliyoachwa na Daniel Chongolo.

Ikirejewa mzizi wa kichama, Katibu Mkuu Chongolo katika zama zake amekuwa akilihimzia hilo kila mara na hata kutishia kufika mbali kuwachukulia wahusika hatua kichama, iwe kwa wahitaji wa nafasi ndani ya chama au kiserikali.

Ikioanishwa tamko hilo, inafungua mlango kwamba sauti ya Chongolo, Mtendaji Mkuu mtagulizi wa CCM, alikuwa akihubiri maelekezo ya Mwenyekiti Dk. Samia, ambaye sehemu kubwa ya wajibu wake inazama katika kuwatumikia Watanzania ofisi ya Ikulu.

Safari ya uchaguzi imefika na Rais Dk. Samia, kaamua kuwarejesha darasani viongozi watokanao na chama chake, kwamba msingi mkubwa kwa mwanasiasa yeyote, wakiwamo viongozo wa chama chake, unazama katika dhana ya kukubalika.

Ni moja ya sababu ikamfanya hata akakemea kile Chongolo alikwishakitolea ufafanuzi mara nyingi, simulizi zenye harufu ya rushwa Dk. Samia akitumia mfano wa 'fedha na kitenge.'

Katika taaluma ya sayansi ya siasa mara zote ina mambo kadhaa inayofikisha mafanikio ya kisiasa, ikiwamo kuhitimishwa dhana ya demokrasia na itifaki kukubalika kwa umma.

Nadharia hiyo inamtaka mwanasiasa au chama chake kuendesha mambo kwa misingi ya utashi wao. Vilevile, kutenda na kuishi katika vigezo wanavyotaka wapigakura na hata wanaoongozwa. Sayansi ya siasa inaweka wazi msingi mkuu unaowavusha kisiasa ni kukubalika, huku wanazuoni wa demokrasia wanahimiza kwamba 'ni utawala wa watu kwa ajili ya watu na kwa manufaa ya watu.'

Vilevile ikifafanua kutoa au kupokea rushwa ni tendo la kuingiza haki katika biashara, kupitia dhuluma ya haki upande mmoja na kumpendelea mnunuzi wa haki hiyo. Mwalimu Julius Nyerere katika zama za uongozi wake alikemea.

> Katika ujumla wake, anachohimiza Rais Dk. Samia ni kujenga demokrasia, haki na uwajibikaji, ili uongozi wake kiserikali na chama- CCM, kufanikisha matarajio yanayozaliwa na kukubalika kisiasa.

"Rushwa ni adui wa haki, wala sitamuonea haya anayepokea au kutoa..." anatamka Mwalimu Nyerere, ambaye katika zama za uongozi wake akatimiza hayo ya ufuatiliaji kufika hata juu ngazi ya Baraza la Mawaziri.

Vyote alilenga kuwapo usafi watendaji wake, hali kadhalika kujenga mfano wa maadili yanayotakiwa, hata kuendelezwa hadi sasa kukiwapo chombo kikubwa kitaifa;Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Pia, Rais Dk. Samia anajenga msingi wa wanasiasa wake CCM kuwajibikia viapo vyao vya uongozi kwa utumishi wa umma wawe wabunge au wawakilishi na vyeo vingine hadi ngazi ya chini, kipato chao kikigharimiwa na kodi ya Watanzania.

Hivyo, anachokinadi Mwenyekiti wa CCM Taifa Rais Dk. Samia, ni ujumbe unaomfikia kila Mtanzania au mwana- CCM au nje ya chama hicho.

Mara zote, kofia ya urais huzunguka nayo daima haimvuki akisafiri na mamlaka, kukirejewa msamiati wa kijeshi 'The Quest of Command is the Commanding Question' kwamba 'rai ya mkuu ni amri.' Hapo inabeba maana rai aliyotoa Dk. Samia Unguja, inasimama kama agizo katika tafsiri pana.

**NAFASI YA KUKUBALIKA**

Kisiasa, Dk. Samia alichohimiza mosi kwa viongozi wateule wa nafasi mbalimbali kupitia kura za wananchi, ni kuwarejesha katika mkataba wao wa msingi kuajiriwa na serikali katika wajibu wao wa msingi (job description) walichukulia viapo.

Mwenyekiti Dk. Samia anawakumbusha viongozi wake wanavyotakiwa kuwajibika, hali kadhalika nadharia ya rushwa ni 'adui wa haki', kwani kadri watakavyowajibika na kuwa wasafi kiutendaji, wanahalalisha kura za waliowateua. Hapo nako kuna kujenga kukubalika kwao, serikali na chama.

Ndani ya mustakabali huo, ikiwa vuguvugu la siasa uchaguzi wa serikali ya mtaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwaka ujao, Rais Dk. Samia anaamini inampa mtaji wa ushindani akiwa na majibu ya walichokifanya katika kipindi kinachopita, pia akijinadi na wagombea wake wakubalike kwa miaka mitano ijayo.

Majumuisho ya yote ndio yanazaa tafsiri ya siasa za nchi ama zina demokrasai au la, ikiwa ni kigezo muhimu cha kukubalika kwa mwanasiasa na chama chake. Ni njia alizotumia Dk. Samia tangu aingie madarakani, akifungua milango ya maridhiano ya kisiasa.

Hapo pakashuhudiwa staili ya kufutia mashtaka ya baadhi ya wanasiasa waliokuwa gerezani, kufungua ulingo wa mijadala kisiasa na wa katiba ya nchi.

Nadharia za sayansi ya siasa zinafafanua kwamba panapo demokrasia, hukaribisha mambo makuu mawili; ridhaa ya umma, vilevile wanahalalisha kilicho utashi wao.

Ndivyo kile alichokuwa anahubiri Rais Dk. Samia kwa viongozi watokanao na kofia ya CCM, tena akizungumza nao kichama, kwa maana ya wanandugu wanaojadili lao barazani mwao, mzazi akikemea watoto 'msituchafue' au 'msiichafue familia.'

Katika ujumla wake, anachohimiza Rais Dk. Samia ni kujenga demokrasia, haki na uwajibikaji, ili uongozi wake kiserikali na chama- CCM, kufanikisha matarajio yanayozaliwa na kukubalika kisiasa.

Nadharia husika inatamka panapo kukubalika kwa ama kiongozi, serikali, chama au vyote kwa pamoja hufika nafasi ya kuipatia mamlaka kuamua na kuelekeza, ikizingatiwa 'kuongoza ni kuonyesha njia.'

Daima kisiasa haiwezekani kuongoza pasipo kukubalika, mara nyingi ndio mwanzo wa utawala wa kiimla.

Hapo mfumo wa kuongoza unapokuwa na mamlaka, sayansi ya siasa inafafanua wenye inakuwa na nguvu ya kutenda, maana iko ndani ya ridhaa, huku katika sura ya pili ikiwajibika inapopaongoza.

Katika kizimba hicho cha demokrasia, wanaoongozwa hujibu kilichomo katika utashi wao katika matumuzi ya kura zao katika ngazi mbalimbali za uchaguzi.

Mtazamo wa jumla ni kwamba, kauli nzito ya Rais Dk. Samia kukemea nyendo za kisiasa ndani ya chama chake kwa watendaji, inaangukia matazamo wa kusafisha CCM, lakini ikifika mbali tafsiri pana ya siasa kitaifa.

Hilo likihamia katika utendaji wa umma, linazama kwa watumishi serikalini na hasa viongozi – waonyeshaji njia akitaka wawajibike kwa mujibu wa hadidu za rejea kuhusu majukumu yao kazini (job descriptions), huku kikubwa zaidi ni anajenga utamaduni mpya wa usafi katika mfumo wa utumishi wa umma.

JUKWAA LA UONGOZI

# Mdudu anapoitafuna, kutishia EAC

• Rwanda, Burundi, Kenya,Uganda, DRC maneno makali kila kona



Rais William Ruto wa Kenya



Rais Evariste Ndayishimiye wa Burundi



Rais Paul Kagame wa Rwanda

**Na Moshi Lusonzo**

MATUKIO ya kutiliana shaka, kutunishiana misuli ya kiuchumi na kutishiana kivita ni baadhi ya mambo yanayoashiria kuyumba kwa sintofahamu miongoni mwa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Mtangamano wa EAC unaoundwa na mataifa nane ya Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokwaria ya Congo, Burundi, Somalia na Sudan Kusini.

Mataifa hayo yamejikuta yakizungukwa na mizozo inayoibuka kila wakati ya kiuchumi na kisiasa, kiasi ambacho kinaanza kuongeza hofu ya hatima ya udhabiti jumuiya hiyo.

Kukosekana maelewano kunahofiwa kuwa kunaondoa dhana halisi ya ushirikiano ndani ya jumuiya hiyo ambayo inakusudia kuwaweka pamoja wananchi, kujenga soko la pamoja lenye nguvu, kusaidiana pale yanapotokea matatizo kwa wanachama na hatimaye kuunda shirikisho la kisiasa lenye serikali moja, sarafu na rais mmoja.

**BURUNDI NA RWANDA**

Mataifa hayo yanayopakana na ambayo raia wake wanaongea lugha moja, yapo katika mzozo ambao matokeo yake yanaweza kuwa mabaya siku zijazo.

Tayari Burundi imefunga mpaka wake na Rwanda, ikiituhumu serikali ya Paul Kagame kuwaunga mkono makundi ya waasi kuanzia yale yanayoishambulia DRC na lile la RED Tabara linalodaiwa linalenga kuiangusha serikali ya Evariste Ndayishimiye.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Burundi, Matin Nitereste, anasema uamuzi wa kufunga mpaka huo unatokana na Rwanda kuwasaidia waasi ambao wanajaribu kupitia mpaka huo kuihujumu nchi yake.

> Kwa miongo kadhaa, Kenya imekuwa ikiagiza mafuta kutoka nje na kuyauza kwa majirani zake wa Afrika Mashariki, lakini Uganda inaonekana kutofurahia utaratibu huo.

Anamnyoonyeshea kidole Rais wa Rwanda, Paul Kagame, kwamba ni jirani 'mbaya' na hivyo wanasitisha uhusiano wote hadi itakapoonekana kuna juhudi za kufikia maelewano.

Hivi karibuni Rwanda imetoa tamko kulaani matamshi yanayotolewa na Rais wa Burundi Evariste Ndayishimiye, na kudai yanahatarisha umoja wa wananchi wake.

Taarifa hiyo kwa vyombo vya habari inasema raia wa Rwanda wanafanya bidii kuimarisha umoja na kujipatia maendeleo na endapo mtu yeyote anajaribu kuwataka vijana wa taifa hilo kupindua serikali yao inakera.

Katika mkutano wake na vijana nchini DRC, Rais Ndayishimiye anaikosoa Rwanda kwa kusaidia makundi yanayovuruga amani eneo hilo.

Rais Ndayishimiye anaongeza kwamba ni muhimu kuendeleza mapambano hadi watu wa Rwanda wenyewe waanze kuweka shinikizo.

Wapo wanaodhani mgogoro wa nchi hizo mbili unatokana na ushiriki wao katika vita vinavyoendelea mashariki mwa DRC na kuwapinga vikali.

Katika mgogoro huo, Burundi inashutumiwa kusaidia kijeshi serikali ya DRC na Rwanda inalaumiwa kwa kuwaunga mkono waasi wa M23 ambao wameteka sehemu muhimu ya mkoa wa Kivu Kaskazini.

Waasi wa M23 wamejiondoa katika maeneo waliyokuwa wameyateka katika mapigano ya hivi majuzi na jeshi katika jimbo la Kivu Kaskazini la DR Congo.

Msemaji wa waasi hao, Meja Willy Ngoma, anaiambia BBC kwamba "tumeondoka katika maeneo hayo ili kufanya amani".

Haijabainika ni wapi waasi hao wamekimbilia, lakini Radio Okapi inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa inasema wamekimbilia karibu na mpaka wa Rwanda.

Machi mwaka jana , Jeshi la DR Congo (FARDC) lilisema kuwa wapiganaji wa M23 wakisaidiwa na Jeshi la Rwanda walishambulia milima ya Chanzu na Runyoni huko Rutshuru.

Msemaji wa Jeshi la Rwanda (RDF) Brigidea Jenerali Sylvain Ekenge, msemaji wa serikali huko Kivu Kaskazini, anawaambia waandishi wa habari kwamba wanaume wawili waliovalia mavazi ya kiraia wametambuliwa kuwa wanajeshi wa Rwanda waliokamatwa na wapiganaji wa M23.

**MOTO WA MAFUTA**

Hali si shwari kati ya mataifa ya Kenya na Uganda baada ya Novemba mwaka jana kuibuka mzozo mkali kuhusu uagizaji na usambazaji wa mafuta kutoka Kenya yanayopitia bandari ya Mombasa.

Uganda ambayo haina bandari, inataka kuagiza mafuta yenyewe bila kuwatumia mawakala kutoka Kenya, lakini nchi hiyo inakataa mpango huo.

Kutokana na hatua hiyo, Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, anakasirishwa na maamuzi hayo na kueleza kuwa nchi yake inadanganywa na wafanyabiashara wanaojigeuza mawakala.

Kwa miongo kadhaa, Kenya imekuwa ikiagiza mafuta kutoka nje na kuyauza kwa majirani zake wa Afrika Mashariki, lakini Uganda inaonekana kutofurahia utaratibu huo.

Rais Museveni anawashutumu wafanyabiashara hao wa kati wa Kenya kwa kupandisha bei ya mafuta hadi kufikia asilimia 58.

Wakati Rais Museveni akitoa kauli hiyo, Bunge la Uganda limeidhinisha uamuzi wa kusitisha uagizaji mafuta kutoka Kenya na kueleza serikali imeweka wazi kuwa inataka uhuru zaidi wa mikataba ya kuagiza mafuta.

Nchi hiyo sasa imegeukia kuagiza mafuta kupitia bandari ya Dar es Salaam na kuiacha ile ya Mombasa.

**VITA ATCL,KQ**

Mgogoro wa hivi karibuni ambao umezidisha joto ndani ya jumuiya hiyo ni ule wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania, kutangaza kusitisha safari za ndege za abiria za Shirika la Ndege la Kenya (KQ).

Hatua hiyo, inakuja baada ya Mamlaka ya Ndege ya Kenya kukataa ombi la Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) kuruhusu ndege ya mizigo kusafirisha shehena kutoka Nairobi kwenda mataifa mengine.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Anga, Hamza Johari, anaiambia BBC kuwa, uamuzi wa Tanzania unatokana na vikwazo vinavyowekwa na mamlaka za Kenya kuzuia shughuli za ndege ya mizigo ya Air Tanzania.

Johari anasema:"Sababu za kuzuia ndege zao ni za msingi, KQ inakuja Tanzania bila vikwazo, lakini sisi ndege yetu ya Air Tanzania inawekewa vikwazo kinyume na makubaliano yetu ya kibiashara ya huduma za ndege tuliyosaini Novemba mwaka 2016. Mkurugenzi anaongeza kuwa wamekuwa wakitafuta mamlaka hiyo ya Kenya kwa ajili ya usuluhishi bila mafanikio.

Mwaka 2020, mamlaka za Tanzania zilisimamisha safari za KQ kati ya Nairobi na ar es Salaam, Kilimanjaro na Zanzibar kwa kile kilichodaiwa kuwa Kenya iliiwekea vikwazo mbalimbali vya kibiashara.

Mzozo huo sasa umetatuliwa na sasa ndege zinaendelea na safari kama ilivyokuwa mwanzo.

**DW, BBC na RFI**



## Kampuni yatoa msaada taulo za kike kukabili upungufu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Afya imesema upungufu wa pedi salama kwa matumizi ya wasichana na wanawake kumesababisha kundi hilo kutumia bidhaa zisiso salama ikiwamo nguo kuku, karatasi, magazeti na majani.

Hayo yalisemwa juzi na Naibu Waziri wa Afya Dk. Godwin Mollel katika hotuba yake iliyosomwa na Mkurugenzi wa Huduma za Tiba Wizara ya Afya, Prof. Pascal Rugajo, wakati akipokea pedi zilizotolewa na Kampuni ya Halotel.

"Changamoto nyingine ni imani zilizopitwa na wakati ambapo suala la hedhi huonekana kama mikosi au laana katika jamii," alisema Dk. Mollel.

Alisema pia suala la hedhi limezungukwa na usiri mkubwa kiasi kwamba jamii inakosa fursa ya kujadili kwa uwazi namna ya kuliboresha kuanzia ngazi ya kaya hadi kwenye taasisi.

Alisema elimu inahitajika zaidi kwa jamii ili kuona suala hilo ni baraka na sio laana au mikosi.

Kadhalika, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Jukwaa la Hedhi Salama imekuwa ikichukua hatua za kukabiliana na changamoto hizo ikwa ni kuanzishwa kwa kampeni ya kuchangia pedi kwa wanafunzi yenye kauli mbiu ya 'Pedi Yangu Afya Yangu'.

Vile vile, alisema lengo ni kugawa pedi milioni tano katika shule za msingi na sekondari nchini.

Alisema wamepokea paketi 2,952 sawa na pedi 29,520 kutoka Halotel ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa kampeni hiyo.

Alisema pedi hizo zitasambazwa katika shule za Mkoa wa Dodoma kwa kuanzia na zitaendelea kugaiwa kwa wasichana waliopo shuleni kwa kadri zitakavyopatikana.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Kinga wa wizara hiyo, Dk. Tumaini Haonga, alisema wamelenga kukusanya pedi zisisopungua milioni tano ambazo zitagaiwa kwa wasichana milioni 1.8 ambao wapo katika shule za msingi na sekondari nchini.

**Alisema wamepokea paketi 2,952 sawa na pedi 29,520 kutoka Halotel ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa kampeni hiyo.**

# Wazazi watakiwa kuwalinda watoto wao dhidi ya ukatili

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

WIZARA ya Katiba na Sheria, imewataka wazazi kuwalinda watoto wao dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na kuacha tabia ya kumaliza kesi nyumbani inapobainika mtoto kafanyiwa ukatili na ndugu wa karibu na familia.

Gladness Msemwa, kutoka wizara hiyo alisema hayo juzi wakati akitoa elimu ya masuala ya haki za watoto pamoja na ukatili wa kijinsia katika Shule ya Sekondari Nkinto na Shule ya Msingi Makulo, Kata ya Nkinto, wilayani Mkalama mkoani Singida ikiwa ni mwendelezo wa kutoa elimu ya kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Compaign).

Alisema kitendo cha baadhi ya wazazi kupenda kumaliza kesi nyumbani watoto wao wanapofanyiwa ukatili ni kuendelea kulea na kumkumbatia waovu wanaoharibu taifa la kesho.

Msemwa alisema Wizara ya Katiba na Sheria imeanza kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia katika nyanja mbalimbali ikiwapo shuleni kwa kuwa maeneo hayo watoto wanafanyiwa vitendo vya kikatili na kutishia mstakabali wa maisha yao ya baadaye.

Alisema ni vyema wazazi kujenga urafiki na watoto wao ili kujua maendeleo yao au kuwaambia mambo wanayofanyiwa pia kuhakikisha wanawalinda dhidi ya vitendo vya kikatili.

Aidha, Msemwa aliwataka watoto kutambua haki zao za msingi ikiwa ni pamoja na haki ya kuishi, kupata elimu, kuendelezwa pamoja na kulindwa huku akiwasihi kutoa taarifa wanapohisi kuna viashiria au vitendo vya ukatili katika familia, jamii na shuleni.

"Kuna wengine mnafanyiwa ukatili majumbani mwenu, shuleni na hata kwenye jamii au ndugu wa karibu, lakini mnaogopa kutoa taarifa unajikuta kama ni mtoto wa kiume unalawitiwa hadi unaharibika sawa na watoto wa kike inasababisha kuathirika kisaikoloji, lakini hamsemi ili msaidiwe kwa kuhofia kuuliwa au kwa vile anakupa vizawadi," alisema.

Alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia ambavyo vimekithiri katika baadhi ya mikoa vinawaacha watoto na matatizo makubwa katika miili yao akili pamoja na kuwaharibu kihisia jambo ambalo serikali haitakubali na hivyo imejipanga kupambana na waharifu wa aina hiyo.

Wanafunzi Musa Christopher na Naomi Matemanga wa kidato cha nne Shule ya Sekondari Nkinto, walimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kupitia kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Compaign), kufika shuleni kwao na kutoa elimu juu ya masuala ya haki za watoto pamoja na ukatili wa kijinsia.

Walisema elimu waliyoipata itawasaidia kuibua vitendo vya kikatili kwenye maeneo yao pamoja na kuwa mabalozi wazuri kwa wengine ili kukomesha tabia hiyo ambayo inawaadhiri wanafunzi kimasomo.



Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge hesaba za serikali za mitaa (LAAC) Halima Mdee akiongoza kamati hiyo Bungeni Dodoma jana ,kamati mbalimbali za Bunge zinaendelea na vikao vyake. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Wanufaika BBT watakiwa kushawishi wengine waingie

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Joyce Ndalichako, amewataka vijana wanufaika wa Mradi wa Jenga Kesho iliyobora (BBT), kutumia nafasi waliyopata kutekeleza mradi huo kwa ufanisi ili kuwashawishi wengine waingie katika kilimo.

Prof. Ndalichako aliyasema hayo jana wakati akipokea vifaa kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) vitakavyotumika kuwasaidia vijana hao kwenye shughuli za kilimo.

Alisema ofisi hiyo kupitia Kitengo cha Huduma za Ajira (TAESA) itatoa fedha za kujikimu kila mwezi Sh.150,000 kwa muda wa miezi sita wakati wakianza uzalishaji.

"Leo mmepatiwa vifaa kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) ili kuwasaidia vijana kwenye shughuli za kilimo, mmekabidhiwa rasmi hati za mashamba nawaasa mkajitume msibweteke ili mjikwamue kiuchumi," alisema.

Alisema wizara yake inahusika na vijana, ataendelea kuwafuatilia, huku akisisitiza fedha watakazopata wajiandae kuandaa makazi yao kwenye viwanja ambavyo watakabidhiwa kwa sababu eneo hilo litatumika kwa vijana wengine.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alisema fedha za kujikimu kwa ajili ya kuwalipa vijana hao zimeshaingia na kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kutelezwa mradi huo.

Alisema tayari kuna vijana 106 ambao walikuwa na ardhi yao wamekopeshwa fedha na wanaendelea na kilimo katika maeneo mbalimbali.

Aidha, alisema vijana 268, katika mashamba ambayo wamekabidhiwa watalima zao la alizeti huku akisisitiza tayari mnunuzi wa zao hilo yupo anasubiri msimu wa kuvuna.

"Hakutakuwa na tatizo lolote la soko kwenye kilimo wanachokwenda kufanya hivyo vijana hao wanauhakika na soko la zao la alizeti ambalo wanakwenda kulima," alisema Bashe.

Hata hivyo, alisema programu hiyo inahitaji mtaji mkubwa na serikali inaendelea kuwasaidia vijana ambao ni wakulima wapya wanaoingia kufanya kilimo biashara nchini.

Alisema, zimeshatengwa Dola za Marekani milioni 610 kwa awamu ya kwanza wameshapokea Dola milion 156 kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Awali, Mkurugenzi wa TADB, Frank Nyabundege, alisema wametoa vifaa hivyo kwa sababu serikali ilitoa mtaji kwenye benki hiyo, Sh. billion 208 ambazo hutumika kwa ajili ya kukopesha na shughuli nyingine.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema amefurahi kuona amepata wakulima ambao wanakwenda kuongeza uchumi wa mkoa wake.





# Tanzania kuzindua mradi kuongeza uzalishaji mpunga

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

TANZANIA inatarajia kuongeza tija ya uzalishaji wa mpunga kutoka tani mbili kwa hekta moja mpaka 10 baada ya kuzinduliwa mradi maalumu unaolenga kuzalisha mbegu bora na kuzigawa kwa wakulima katika maeneo mbalimbali nchini.

Mradi huo pia unakusudia kupanua eneo linalolimwa zao hilo nchini ili kupata mazao mengi zaidi yatakayofanya Tanzania kujitosheleza kwa chakula na kuwa muuzaji wa mchele nje ya nchi.

Aidha, unalenga kutoa elimu ya mbinu bora za uzalishaji wa mpunga kwa wakulima na wadau mbalimbali wa kilimo ili kufikia malengo ya kuongeza uzalishaji.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Dk. Geofrey Mkamilo aliyasema hayo juzi jijini hapa wakati wa uzinduzi wa mradi huo ambao unasimamiwa na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mpunga (IRRI).

Alisema kwa sasa Tanzania ina eneo lenye ukubwa wa zaidi ya hekta milioni 21, zinazofaa kwa kilimo cha mpunga, lakini zinazotumika ni hekta milioni 1.7 pekee na kwamba eneo kubwa bado halijaanza kutumika.

Alisema kiasi cha mchele unaozalishwa nchini ni tani milioni nne, lakini zinazotumika nchini ni milioni 1.5 mpaka tani milioni mbili na kwamba mradi uliozinduliwa utasaidia kuongeza eneo la uzalishaji na tija.

"Tija yetu ni ndogo sana ukilinganisha na mataifa mengine, sisi kwa sasa tija yetu ni tani 1.5 mpaka mbili kwa hekta wakati mataifa mengine kama Misri tija yao ni tani 10, kwahiyo tunaamini mradi huu utatusaidia sana," alisema Dk. Mkamilo.

Mratibu wa mradi huo Nyanda za Juu Kusini, Dk. Dennis Tippe, alisema kwenye uzinduzi wa mradi huo walishiriki watafiti wa kilimo kutoka katika mataifa 17 duniani.

Alisema mradi wa utafiti wa mpunga umefanyika kwa mara ya kwanza nchini Tanzania kwa maelezo kuwa utafiti mwingine umezinduliwa kwenye mataifa mengine.

Alisema kwenye mradi huo wanakusudia kuanza uzalishaji wa mbegu bora na za kisasa ambazo zina tija kubwa kwenye uzalishaji na zinaendana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaikumba dunia kwa sasa.

"Tunataka hapa katika kituo cha TARI Uyole tuanzishe mashamba darasa ambayo tutakuwa tunayatumia kuwafundisha wakulima na maofisa ugani kuhusu teknolojia mbalimbali za uzalishaji wa mpunga kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini," alisema Dk. Tippe.

Mwakilishi wa IRRI kwenye uzinduzi wa mradi huo, Dk. Ajay Panchbhai, alisema waliamua kuzindua mradi huo katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwa sababu ndio ukanda unaozalisha mpunga kwa kiwango kikubwa.

Alisema ukanda huo unachangia zaidi ya asilimia 40 ya mpunga wote unaozalishwa nchini na ni ukanda muhimu zaidi kuliko kanda zingine.

Akizindua mradi huo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema mradi huo utasaidia kufikia malengo ya ajenda 10/30 ambayo inalenga kuongeza uzalishaji kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ndiyo inaongoza kwa uzalishaji wa chakula nchini hali liyoifanya kubaitzwa jina la 'ghala la taifa la chakula'.



Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa akizungumza na Wananchi wa kata ya Ipelele mara baada ya kukagua ujenzi wa barabara ya Isyonje - Kitondo - Makete sehemu ya Kitulo - Iniho (km36.3) kwa kiwango cha lami, Mkoani Njombe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bashungwa ampa mkandarasi wiki tatu za kutekeleza mradi

**Na Elizabeth John,**
MAKETE

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa ametoa wiki tatu kwa mkandarasi Kampuni ya China National Aero Technology International Engineearing Corporation anayejenga barabara ya Isyonje-Kikondo-Makete (km 96.2) kwa kiwango cha lami kuanza utekelezaji wa mradi.

Mradi huo una thamani ya zaidi ya Sh. Bilioni 80 na unalenga kuunganisha mikoa ya Mbeya na Njombe kupitia Hifadhi ya Taifa ya Kitulo.

Alitoa agizo hilo alipotembelea barabara hiyo na kubaini mkandarasi kutoanza ujenzi kwa wakati akiwa nyuma ya muda ambapo alitakiwa kuanza mwezi julai mwaka jana na kutakiwa kukamilika mwezi julai 2026.

Pia waziri aliagiza kuchunguzwa kwa watu wanaohusika na mikataba kwa sababu ya kushindwa kusimamia kikamilifu mikataba inayosainiwa.

"Tunaposaini mikataba ni lazima isimamiwe, na mtendaji mkuu wa TANROADS kitengo cha contract management (mikataba) kama wameshindwa kusimamia fukuzeni wote watanzania wapo wengi wenye taaluma ya kusimamia," alisema Bashungwa.

Hata hivyo Bashungwa alisema Rais Samia Suluhu Hassan alileta fedha ili mkandarasi huyo afanye kazi usiku na mchana na si vyenginevyo.

"Sawa kuna masuala ya mvua lakini wakati wa mvua inanyesha kuna masuala mengine ambayo mnaweza mkafanya, yale ambayo yanahitaji kiangazi yatasubiri kiangazi, mtambo hii lazima ije haraka sana," alisema Bashungwa.

Awali, Kaimu Mkurugenzi wa miradi kutoka Wakala wa Barabara (TANROADS), Japhason Nnko alisema kwa kipindi miezi sita mradi umefika asilimia 4.2 badala ya asilimia 8.4.

"Katika kazi kubwa ambayo imefanyika ni ujenzi kambi ya mkandarasi ambayo imekamilika kwa asilimia 90 lakini kambi ya mwandisi mshauri ambayo imekamilika kwa asilimia 55 lakini pia ameanza kusafisha kwenye barabara ambayo jumla ndiyo hii asilimia 4.2 na mkandarasi ameshalipwa malipo ya awali ile asilimia 10," alisema Nnko.

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Makambako, Deo Sanga, aliwataka wananchi hao kulinda vifaa ili mradi huo uweze kukamilika kwa wakati.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, alisema ujenzi wa barabara hiyo utawasaidia wananchi hao ambao wanajishughulisha na kilimo cha viazi kusafirisha mazao yao kwenda nje ya mkoa huo.

Katika ziara hiyo, Waziri Bashungwa alitembelea pia barabara ya Njombe-Moronga-Makete (Mizani), barabara ya Kitulo Iniho, barabara ya Ramadhani-Iyayi na barabara ya Chalowe-Ingwachanya.

# Mawakala wanaohujumu mbolea ruzuku waonywa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa amewatahadharisha wakulima na mawakala wa pembejeo za kilimo wanaoshiriki kuhujumu mfumo wa mbolea ya ruzuku akisisitiza kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Malisa alitoa tahadhari hiyo juzi kwenye kikao kilicholenga kujadili mambo mbalimbali yanayohusu pembejeo za kilimo na kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo mawakala wa mbolea ya ruzuku, maofisa kilimo pamoja na wakaguzi wa mbolea kilichofanyika jijini hapa.

Alisema serikali itawachukulia hatua kali wakulima wanaokubali taarifa zao zitumike katika kufanya udanganyifu kwa kuwanufaisha baadhi ya mawakala wa mbolea ya ruzuku wasio waaminifu kwani kufanya hivyo ni kuhujumu zoezi la mbolea hiyo lenye malengo chanya kwa wakulima nchini.

"Wakulima wamekuwa chanzo kikubwa cha kuwasaidia mawakala kufanya udanganyifu kwenye zoezi la mbolea ya ruzuku, natoa onyo kuacha tabia hiyo mara moja kwani haikubaliki na inarudisha nyuma jitihada za Serikali kuwasaidia wakulima kupata mbolea kwa bei nafuu," alisema Malisa.

Aliwataka wakulima kutumia vizuri fursa ya kutumia mbolea ya ruzuku inayotolewa na serikali yenye malengo ya kuongeza tija katika kilimo sambamba na kumuongezea kipato mkulima.

Aliongeza kuwa hadi sasa wakulima 135,635 wamejitokeza kujisajili na kuhuisha taarifa zao katika mfumo wa mbolea ya ruzuku katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Maofisa kilimo pamoja na wakaguzi wa mbolea walioshiriki kikao hicho waliahidi kusimamia vema zoezi la utoaji wa mbolea ya ruzuku katika Halmashauri yao ili kuhakikisha wakulima wananufaika na mbolea hiyo sawa na malengo ya Serikali ili kuongeza tija ya uzalishaji wa kilimo Nchini.

Hata hivyo, ofisa kilimo kutoka kampuni ya Hakika ambao ni wasambazaji na wauzaji wa Mbolea ya ruzuku, Hamisi Kilanga, aliomba serikali kutoa elimu ya kutosha kwenye mfumo wa sasa umaotumika kwasababu mara nyingi umejitokeza usumbufu pale ujumbe wa mfumo unaposhindwa kurudisha ujumbe ili mteja aweze kupewa mbolea.



# Mradi usimamizi uvuvi kunufaika Dola mil. 112

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JUMLA ya dola za Kimarekani milioni 112 zinatarajiwa kutumika katika mradi wa usimamizi wa uvuvi na mazao ya baharini (Pre appraisal mission) unaosimamiwa na Benki ya Dunia chini ya usimamizi wa mradi wa TASFAM.

KATIBU Mkuu Wizara ya Uvuvi na Mifugo, Riziki Shemdoe, alisema hayo jana visiwani hapa katika mkutano uliowashirikisha wadau kutoka taasisi zinazosimamia mradi huo nchini.

Alisema fedha hizo zitatumika kwa ujenzi wa miundombinu ya taasisi zinazohusika na ufundishaji taaluma ya uvuvi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na mradi huo.

Pia, mradi huo utaongeza mafanikio kwenye sekta ya uvuvi ambayo inachangia asilimia 1.7 kwenye Pato la Taifa na lengo baada ya mradi kufikia asilimia tano.

"Wengi watanufaika na mradi huu hasa vijana na kinamama kwa ajili ya kupata kipato kupitia sekta ya uvuvi," alisema.

Aidha, utawasaidia wavuvi na watumiaji wa bahari wakiwamo wakulima wa mwani na wafugaji wa majongoo kutumia vyema bahari kuona thamani inayotumika kwenye mradi huo unaleta tija kwa wananchi.

Aliwataka wasimamizi wa mradi huo kutumia vyema fedha za miradi kwa maslahi ya taifa na wananchi kunufaika na miradi inayoazishwa.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema mradi huo umekuja kutokana na kumalizika kwa miradi ya Massemp na Siofish ambayo ilileta matukeo mazuri katika kukuza sekta ya uvuvi na kuleta mafanikio zaidi ya kiuchumi.

"Kuwapo kwa ushirikiano mzuri kati ya Tanzania na Benki ya Dunia ndio maana wakaleta mradi huo ili kuwasaida wananchi wanaojihusisha na utumiaji wa bahari," alisema.

Alisema sekta ya uvuvi inakua kwa kasi ya asilimia tisa kwa mwaka na kujumuisha wavuvi wadogo wa samaki wapatao 100,000 Unguja na Pemba.

"Mradi huu pia unalengo la kuimarisha miundombinu na kuongeza kipato kwa wananchi na utakondoisha masuala ya uchumi wa buluu hapa Tanzania na kuvusha uchumi ambao ndio uti wa mgongo wa taifa," alisema.

Alisema mradi huo pia utawahusisha wavuvi wadogo kwa wilaya zote 11 za Unguja ambao watanufaika na mradi huo na utasaidia idara ya uratibu wa uchumi wa buluu kuharakisha kazi ya matayarisho ya mpango mahsusi wa matumizi ya maeneo ya bahari (Marine Spatial Planning) na kuiwezesha kampuni ya uvuvi ya (ZAFICO) kufanya kazi kwa bidii katika mifumo ya kiushindani ya biashara za ndani na nje ya nchi.

Msimamizi wa masuala ya mazingira wa mradi huo, Dk. Enos Esikuri, alisema utekelezaji wa mradi ni kwenda sambamba na dira ya maendeleo ya mwaka 2050, mpango wa maendeleo wa ZADEP pamoja na ilani ya Chama cha Mapinduzi na utekelezaji wa sera ya uchumi wa buluu.

Mradi huo wa miaka mitano unatekelezwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi Tanzania Bara, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Mamlaka ya usimamizi wa bahari kuu Tanzania, pamoja na mradi wa TASFAM wa Benki ya Dunia.



Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Dk. Mngereza Mzee Miraji, akizungumza na ujumbe kutoka European Mortgage Federation na taasisi inayoshughulikia masuala ya mikopo ya ujenzi wa nyumba ya Dar es Salaam (TMRC) wakati walipofika jana katika Ofisi za Wizara ya Ardhi iliyopo Maisara Zanzibar. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Madrasa yafungiwa madai ya kukashifu viongozi

**Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

OFISI ya Mufti Mkuu wa Zanzibar imeifungia Madrasa Tawhid ya Kidoti, Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa madai ya kutoa matamshi ya kukashifu viongozi pamoja na kupiga nyimbo zinazokwenda kinyume na maadili.

Akitoa taarifa hiyo kwa waandishi wa habari jana visiwani humo, Mkurugenzi wa usajili katika ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar, Abdul Simai Khamis, alisema uongozi wa madrasa hiyo umekwenda kinyume na maagizo na maelekezo ya Ofisi ya Mufti katika uendeshaji wa madrasa za Quran.

Alisema Ofisi ya Mufti ilitoa onyo na karipio kuacha kuchanganya Qasida pamoja na nyimbo za taarab na bongo fleva, utaratibu ambao haukubaliki.

Alisema kufanya hivyo ni kwenda kinyume na maadili na utamaduni wa kisomo cha Qasida ambacho kinahusisha sifa zenye mwelekeo wa kidini.

"Madrasa hii tumeifunga kwa sababu hizo ambapo hivi sasa utaratibu wa kisomo cha Qasida unakiukwa ambapo nyimbo za bongo fleva pamoja na taarabu zinachanganywa kwa pamoja na hivyo kuleta taswira mbaya," alisema.

Aidha, aliitaka jamii kuzingatia mila na tamaduni wakati wanapofanya sherehe mbalimbali ikiwamo za harusi na kutokiuka maadili ya kidini.

**Alisema Ofisi ya Mufti ilitoa onyo na karipio kuacha kuchanganya Qasida pamoja na nyimbo za taarab na bongo fleva, utaratibu ambao haukubaliki.**

# 'SMZ imeweka mazingira rafiki marekebisho ya sheria'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Dk. Mngereza Mzee Miraji, amesema Serikali ya Zanzibar imeweka mazingira rafiki kwa kuzifanyia marekebisho sheria zake ili kutoa fursa kwa wawekezaji kuja kuwekeza Zanzibar.

Aliyasema hayo jana katika mazungumzo maalum yaliowashirikisha ujumbe kutoka European Mortgage Federation na taasisi inayoshughulikia masuala ya mikopo ya ujenzi wa nyumba ya Dar es Salam (TMRC) wakati walipofika katika Ofisi za Wizara ya Ardhi, Maisara Zanzibar.

Dk. Mngereza alisema Serikali ya Zanzibar imefungua milango yake kwa kuwakaribisha wawekezaji kuwekeza katika ardhi ya Zanzibar huku sheria na sera masuala ya uwekezaji zikiwa zimeimarishwa.

Alisema, dhamira ya ujumbe huo kutaka kufanya mkutano wa kimataifa Zanzibar ni njema na serikali kupitia Wizara ya Ardhi itatoa kila aina ya ushirikiano katika kufanikisha azma hiyo.

Alisema ujumbe huo uliofika unakwenda sambamba na dhamira ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi wa kutaka kuifanya Zanzibar kuwa kituo kikuu cha kufanyia mikutano ya kimataifa ya kitalii.

"Serikali ya awamu ya nane inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Mwinyi imedhamiria kuimarisha uchumi wake kwa kuanzisha utalii wa mikutano," alisema Dk. Mngereza.

Pia, alisema Zanzibar imebarikiwa kuwa na fukwe nzuri pamoja na maeneo ya kihistoria jambo ambalo wageni watakaofika Zanzibar watafurahia kwa kuyatembelea maeneo hayo kwa kupata maelezo ya kihistoria.

Katibu Mkuu wa European MortgageFederation, Luca Bertolt, alisema wamekusudia kufanya mkutano wa kimataifa Zanzibar utakaowashirikisha wawekezaji kutoka nchi mbalimbali duniani.

Alisema kufanyika kwa mkutano huo kutafungua fursa muhimu kibiashara kwa watu wa Zanzibar pamoja na kuitangaza nchi kimataifa.

Mtendaji Mkuu kutoka taasisi inayoshughulikia masuala ya mikopo ya nyumba (TMRC) kutoka Dar es Salam alisema kupitia mkutano huo unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu,

Zanzibar inaweza kupata wawekezaji ambao watajenga nyumba za bei nafuu huku ikiendelea kupendezesha mji wake kwa kuwa na majengo mazuri.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MWANASHA JUMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0468/0058 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIRIKI HIGH SCHOOL MWANGA KILIMANJARO** mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **RB/ PHQ/MBE/MBE/1453/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LAURENT E. MARISHAMU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0160-0109 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia UMBWE SEKONDARI mwaka 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MSI/RB/423079/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NURU JULIUS MAIRI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S3933-0014 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia RISING STAR SEKONDARI November, 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MWA/NYA/11142/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MIKA EDWARD TEMI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4980-0044** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ILANDAMILUMBA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2018.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: DAR/KIG/RB/20459/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No 1154 of 2024**
**In the matter of the estate of the late MARIETHA CHARLES IPINI of Dodoma within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letter of administration by LEAH CHARLES IPINI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.


Objections to the grant should be filed on or before the 21 day of FEBRUARY .........2024

Dated at Dodoma this 22ND day of JANUARY......2024

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE I/C, DODOMA DISTRICT

.......................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HENRY FRAYSON SIMBEYE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0757.0511 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KYELA SECONDARY SCHOOL mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/ILA/9844/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JACOB LEONARD MAKELE**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari(MISTUBISH CANTER) yenye namba za usajili T 500DXH, Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**PHQ/MOR/MOR/1583/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...05/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: PETER AMANDUS MNJELU wa KILAKALA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA SIJAL PETER NICHOLAUS**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 29 Mwezi 01 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 15 mwezi 01 mwaka 2024

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EVELYNE ITANISA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI T 889 AVQ, CHASIS NUMBER GRX1200034656. YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI **TAARIFA PHQ/IRI/IRI/970/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RICHARD OTHINIEL JAFFU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 655 CYX aina ya Toyota NOAH.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOD/DOD/RB/74063/2023.**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701*

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rwanda yamshutumu rais wa Burundi

**KIGALI,** Rwanda

SERIKALI ya Rwanda imeshtumu matamshi yaliyotolewa na Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye (pichani), ikieleza kuwa matamshi hayo yasiyokuwa na msingi yalilenga kuchochea mgawanyiko nchini Rwanda kwa kuzua ghasia na kuharibu amani katika eneo lote la maziwa makuu.

Katika mahojiano na vijana yaliyofanyika Kinshasa, nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) Rais Ndayishimiye alikosoa mamlaka ya Rwanda kwa kusaidia makundi yanayovuruga eneo hilo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana, raia wa Rwanda walifanya bidii kuimarisha umoja na maendeleo, ikisisitiza kwamba kitendo cha mtu yoyote kujaribu kuwataka vijana wa taifa hilo kupindua serikali yao ni jambo lisilokubalika.

Iliongezea kwamba inakera zaidi kwa kiongozi jirani kutoa matamshi kama hayo katika hafla ya Umoja wa Afrika (AU) suala ambalo ni ukiukaji wa mkataba wa umoja huo.



Hata hivyo taarifa hiyo ilieleza kwamba taifa la Rwanda halina haja ya kuzua ghasia na majirani zake na kwamba litaendelea kushirikiana nao katika eneo hilo na kwingineko ili kuimarisha udhibiti na maendeleo.

Ndayishimiye pia alisema kwamba ni muhimu kuendeleza mapambano hadi watu wa Rwanda wenyewe waanze kutoa shinikizo, huku akieleza kuwa anadhani vijana wa Rwanda hawawezi kukubali kuwa wafungwa katika eneo hilo.

Inaelezwa kuwa utawala wa Gitega umekuwa ukiitizama Kigali kwa jicho baya tangu mwishoni mwa mwaka jana walipoishutumu Rwanda kwa kusaidia kundi la RED-Tabara lililofanya shambulio baya kaskazini na magharibi mwa Burundi.

Serikali ya Rwanda ilisema haina uhusiano wowote na shambulio hilo. Na baada ya muda serikali ya Burundi ilifunga mpaka wake na Rwanda. **BBC**

# Israel yakubali kusitisha mapigano miezi miwili

**TEL AVIV,** Israel

ISRAEL inaripotiwa kuwa tayari na pendekezo la kusitisha mapigano ya miezi miwili ambayo yanalenga kuhakikisha kuachiliwa kwa mateka wanaoshikiliwa na Hamas na makundi mengine lakini bila kumaliza vita huko Gaza.

Vyombo vya habari vya Marekani na Israel viliripoti jana kuwa Israel ina matumaini kwamba inaweza kukamilisha makubaliano kwa msaada wa Marekani. Ikielezwa kuwa mpango huo unakuja dhidi ya hali ya mapigano makali kusini mwa Gaza pamoja na kuongeza shinikizo kwa serikali ya Israel kutafuta makubaliano ya kuwarudisha mateka nyumbani.

Inaelezwa kuwa tovuti ya Marekani ya Axios ilinukuu maofisa wa Israel wakisema kuwa pendekezo hilo limewasilishwa kwa Hamas kupitia wapatanishi wa Qatar na Misri. yakijumuisha mapatano ya miezi miwili ambayo wafungwa wote wa Israel huko Gaza wataachiliwa huru.

Idhaa ya 13 ya Israel iliripoti kwamba kanuni za mpango huo zinajumuisha hatua tatu hadi nne za kuachiliwa huru. Na kwamba Jeshi la Israeli lingeondoka kutoka katika baadhi ya maeneo ya eneo hilo, bila kumaliza vita.

Ripoti zinaonyesha kuwa Marekani inasukuma mpango huo na washirika wa kikanda. Huku Mratibu wa Ikulu ya White House ya Mashariki ya Kati, Brett McGurk, akiwa yuko Cairo kujadili mpango huo, na mipango ya kuendelea na Qatar.

**MIPANGO ILIVYO**

Kwa mujibu wa Al Jazeera, pendekezo hilo lilijumuisha mipango ya kuwaachilia mateka kwa awamu, kuanzia wanawake na wale walio na umri wa zaidi ya miaka 60.

Awamu ya pili itahusisha makabidhiano ya askari wa kike na wanaume wanaochukuliwa kuwa wasio wanajeshi na Hamas. Awamu ya tatu itajumuisha wanajeshi wa kiume na miili iliyosalia ndani ya Gaza.

Aidha, ilielezwa kuwa wanajeshi wa Israel wanaweza kutumwa tena mbali na baadhi ya maeneo ya mijini ili kuwaruhusu Wapalestina kurejea nyumbani.

Awali makubaliano ya mwezi Novemba 2023 ylihusisha kuachiliwa huru takriban mateka 100 kati ya 240 au zaidi waliopelekwa Gaza Oktoba 7, wakati Hamas ilipoanzisha mashambulizi ya kushtukiza ndani ya Israel, na kwamba juhudi za kusitisha mapigano zimekuwa za kigugumizi tangu wakati huo.

Jumuiya ya Hilali Nyekundu ya Palestina ilisema mapema kwamba makao makuu yake huko Khan Younis yamepigwa makombora.

Ikiandika kwenye X, ilisema kwamba ufyatuaji wa makombora uliambatana na milio ya risasi kutoka kwa ndege zisizo na rubani za Israeli, na kusababisha majeraha kati ya wakimbizi wa ndani ambao walitafuta usalama kwenye majengo yao.

Mashirika ya Umoja wa Mataifa na mashirika ya misaada yametoa hofu kuhusu tishio linaloongezeka la magonjwa na njaa huko Gaza, ambayo watu milioni 1.7 wanakadiriwa kuwa wameyahama makazi yao.

Vile vile jeshi la Israel liliripoti kuwa limepoteza takriban wanajeshi 21 katika moja ya mashambulizi mabaya zaidi dhidi ya wanajeshi wake tangu vita hivyo vilipoanza miezi mitatu iliyopita. **ALJAZEERA**



Familia za mateka waliowekwa kizuizini na Hamas wakiandamana huko Israel wakitaka wapendwa wao waachiliwe. **PICHA: MTANDAO**

# Uturuki yapiga kura kuridhia Sweden kujiunga NATO

**ANKARA,** Uturuki

BUNGE la Uturuki limepiga kura kuidhinisha Sweden kuingia katika Muungano wa Kujihami wa (NATO) baada ya kucheleweshwa kwa hatua hiyo kwa zaidi ya mwaka mmoja.

Inaelezwa kuwa kura hizo zimepigwa jana, na kwamba uamuzi huo unakuja baada ya tume inayohusika na Mambo ya Nje ya Uturuki kuidhinisha ombi la nchi hiyo kuwa mwanachama mwezi uliopita.

Inaelezwa kuwa mwaka 2022, Sweden na Finland zilituma maombi ya kutaka kuwa wanachama wa muungano huo. Na kwamba Finland hatimaye ilijiunga NATO Aprili 2023, huku ikibainishwa kuwa Uturuki ilikataa kuidhinisha ombi la Sweden, uamuzi ambao umekatisha tamaa washirika wake wa Magharibi.

Hapo awali, Uturuki ilikataa kuidhinisha uanachama wa Sweden kwa madai kwamba nchi hiyo iliunga mkono wanachama wa Chama cha Wafanyakazi wa Kurdistan (PKK), ambacho kinatambuliwa kama kundi la kigaidi na Uturuki, Umoja wa Ulaya na Marekani.

Inaelezwa kuwa tangu wakati huo Sweden imeandaa mswada wa kupambana na ugaidi unaofanya uanachama wa kundi lolote la kigaidi kuwa kinyume cha sheria. **VOA**

# KOCHA YANGA PRINCESS ATOA SABABU KUPOTEZA 3 MFULULIZO

**Na Saada Akida**

MAKOSA binafsi ya wachezaji wa Yanga Princess ndio sababu ya kupoteza mchezo wa juzi wa Ligi Kuu ya Wanawake nchini dhidi JKT Queens, kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Charles Haalubono.

Yanga imepoteza alama tisa katika michezo mitatu mfululizo ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, iliacha alama dhidi ya watani wao, Simba Queens, Ceasiaa Queens na juzi kukubali kichapo cha mabao 1- 3 kutoka kwa JKT Queens, mchezo ukipigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

**Akizungumza baada ya dakika 90 kukamilika, Kocha Haalubono alisema hana furaha kwa kupoteza mechi ya tatu mfululizo na kushindwa kutumia nafasi zinazopatikana kutokana na makosa ya mchezaji mmoja mmoja.**

Aliwapongeza JKT Queens kwa kuonyesha ushindani mkubwa na kucheza mchezo mzuri, hivyo kufanikiwa kutumia makosa yao kwa kupata ushindi.

"Haikuwa mechi rahisi, wachezaji wangu walipambana na kutengeneza nafasi, lakini tukashindwa kuzitumia, pia makosa ya mchezaji mmoja mmoja yametuadhibu. Tunarudi uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu yetu na kuendelea kuwasisitiza wachezaji wangu kuwa makini," alisema kocha huyo.

Naye nahodha wa Yanga, Irene Kisisa, alisema mechi ilikuwa ngumu, makosa yao yamewaadhibu na benchi la ufundi limeona mapungufu yao hivyo watafanyia kazi katika uwanja wa mazoezi.

"Ni kweli tumepoteza mechi tatu mfululizo sasa, lakini haina maana tumekata tamaa katika mbio za ubingwa, bado ligi ni mbichi ndio kwanza mechi ya tano, tunaenda kujipanga kwa mechi zijazo na tunaimani kuwa tutafanya vizuri," alisema Irene.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Yanga Princess inashika nafasi ya nne ikiwa na alama 10 sawa na Ceasiaa Queens ya Iringa iliyopo nafasi ya tatu huku Simba Queens ikishika nafasi ya pili kutokana na kukusanya alama 13 huku JKT Queens wakiwa kinara wa msimamo huo.



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma maarufu Mwana FA (kushoto), akimkabidhi seti ya jezi Katibu wa CCM Kata ya Mtindiro wilayani Muheza, Salehe Mwinjuma, katika Uwanja wa Jitegemee juzi. Alikabidhi jumla ya jezi 132 pamoja na mipira kwa kila timu ya kijiji katika Jimbo la Muheza na kisha kufungua rasmi mashindano ya mpira wa miguu jimboni hapo yajulikanayo kama MwanaFA Cup. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Ni vita Kiatu cha Dhahabu Championship

**Na Adam Fungamwangwo**

WAKATI timu za Ligi ya Championship zikipambana kuwania kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, kuna vita nyingine inayoendelea ya kuwania ufungaji bora wa ligi hiyo inayoongozwa na Edger William wa KenGold mwenye mabao 15 mpaka sasa.

Kwa mujibu ya takwimu zilizotokewa jana na Bodi ya Ligi, Edger ambaye kwa kiasi kikubwa mabao yake ndiyo yanaisimamisha KenGold juu ya msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 42 kwa michezo 18 iliyocheza, anafuatiwa kwa karibu na straika wa zamani wa Mtibwa Sugar, Mganda Boban Bogere wa Biashara United ambaye mpaka sasa ameshafunga mabao 13, mawili nyuma ya kinara.

Boban anaifanya Biashara United kuwa nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 37.

Straika wa zamani wa Kagera Sugar ambaye kwa sasa anaichezea Mbeya Kwanza, Ramadhani Kapera na Salim Aiyee wa Mbuni FC wako kwenye nafasi ya tatu wakipachika mabao tisa kila mmoja.

Hata hivyo, Aiyee straika wa zamani wa Mwadui, hatokuwa tena sehemu ya wanaowania ufungaji bora kwenye ligi hiyo kwani amesajiliwa na Coastal Union na kurejea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Jumla ya wachezaji watano wapo kwenye nafasi ya nne ya kinyang'anyiro hicho ambao ni Abdulkarim Segeja wa Copco FC, Frank Fransis (TMA FC), Helbert Lukindo (Biashara United), Maulid Shaaban (Mbeya City) na Kassm Shaibu wa KenGold, ambao wote hao wamefunga mabao manane kila mmoja.

## Stumai afunguka kukaa kileleni Ligi Wanawake

**Na Adam Fungamwangwo**

STRAIKA hatari wa JKT Queens, Stumai Abdallah, juzi alifunga bao moja akiipa ushindi wa mabao 3-1 timu yake dhidi ya Yanga Princess na kukaa kileleni mwa orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu ya Soka kwa Wanawake nchini, akimpiku Aisha Mnunka wa Simba Queens.

Stumai, aliyepachika bao dakika ya 42, likiwa la pili kwenye mchezo huo uliochezwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, na kufikisha mabao tisa, amesema anafurahia kila anapofunga bao kwa ajili ya timu yake, lakini nia yake kubwa ni kuona timu yake inatwaa tena ubingwa wa Tanzania Bara, huku suala la kiatu cha dhahabu, akiliweka pembeni kwanza.

"Kwanza mimi ninachotaka timu yangu ichukue ubingwa, ufungaji bora, kiatu cha dhahabu na zawadi nyingine zitakuja tu," alisema Stumai.

Stumai amemzidi bao moja straika wa Simba Queens, Aisha Mnunka, aliyebaki na mabao yake manane, baada ya kushindwa kupata bao katika mechi ya juzi dhidi ya Bunda Queens, timu yake ikilazimishwa suluhu kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

Akizungumzia mchezo huo, Stumai alisema ulikuwa mgumu tofauti na ushindi mkubwa walioupata.

"Mchezo ulikuwa mgumu, zilizocheza ni timu kubwa, zinapokutana hizi, JKT Queens, Simba Queens na Yanga Princess hakuna mechi rahisi, lazima iwe ngumu, ukiwaona jinsi walivyocheza mchezo uliopita na Ceasiaa Queens sivyo walivyocheza leo, walikuja kivingine kabisa, ilibidi wakati mwingine wachezaji tuitane kwa ajili ya kubadilisha mfumo wa uchezaji mara kwa mara.

Katika mechi zingine za Ligi Kuu ya Wanawake zilizochezwa juzi, Alliance ilikubali kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Baobab Queens katika Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza, Fountain Gate Princess ikiwa Uwanja wa Nyankumbu, ililazimisha sare ya mabao 2-2 dhidi ya wenyeji wao, Geita Gold Queens, huku Ceasiaa Queens ikiiadhibu Amani Queen mabao 2-0, mechi ikipigwa Uwanja wa Samora, Iringa.

JKT Queens bado inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 15, Simba Queens ya pili ikiwa na pointi 13, Ceasiaa Queens ya nne ikiwa na pointi 10, Yanga Princess ikishika namba tano kwa pointi zake tisa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WEST HAM NA PHILLIPS

KLABU ya West Ham inakaribia kukubali mkataba wa mkopo na Manchester City kwa Kalvin Phillips, 28, lakini Juventus bado wanaweza kuwasilisha ombi la dakika za mwisho kwa kiungo huyo wa kati wa England. ***(Mail)***

### BROBBERY AITAKA MAN U

MSHAMBULIAJI wa Ajax na Uholanzi, Brian Brobbey, 21, anatamani kujiunga na Manchester United na kufanya kazi na kocha wa zamani wa kikosi hicho, Erik ten Hag. ***(Football Insider)***

### BENZEMA KUREJEA LYON

KLABU ya Lyon inajaribu kumrejesha Karim Benzema, 36, katika klabu hiyo kutoka Al-Ittihad, huku fowadi huyo wa zamani wa Ufaransa akiwa ndiye mchezaji wa hivi punde zaidi wa hadhi ya juu kutaka kuondoka kwenye Ligi Kuu ya Saudi Arabia. ***(Guardian)***

### NEWCASTLE NA EDERSON

NEWCASTLE United haina uwezo wa kumudu dili la kumnunua kiungo wa kati wa Brazil, Ederson, mwezi huu, huku klabu yake ya Atalanta ikimthaminisha kati ya pauni milioni 30 hadi milioni 40. ***(Football Insider)***

### CHELSEA YAMZUIA COLWILL

CHELSEA haina nia ya kumuuza mlinzi wa England, Levi Colwill, 20, mwezi huu licha ya Liverpool kumtaka. ***(TeamTalks)***

### TRIPPIER PAUNI MIL. 12

KLABU ya Newcastle United inaitaka Bayern Munich kulipa ada ya takribani pauni milioni 12 kwa beki wao wa pembeni, Kieran Trippier, 33, ambaye ana nia ya kuhamia Ujerumani. ***(Sky Germany via Sky Sports)***

### ALMIRON SASA KUACHWA

NEWCASTLE pia inaweza kushawishiwa kuachana na mchezaji wa Kimataifa wa Paraguay, Miguel Almiron, 29, huku Klabu ya Al-Shabab inayoshiriki Ligi Kuu ya Saudi Aarabia ikimtaka winga huyo. ***(Guardian)***

### GIBBS-WHITE ATAKIWA

NEWCASTLE United inamuona, Morgan Gibbs-White, 23, kama mbadala mzuri wa Miguel Almiron, lakini Nottingham Forest ina uwezekano wa kukataa kumuuza mchezaji huyo. ***(Telegraph)***

### CHELSEA, UNITED ZAZUIWA

CHELSEA na Manchester United wameambiwa na Nice kwamba, haitakaribisha ofa kwa mlinzi wao wa Kimataifa wa Ufaransa, Jean-Clair Todibo, 24, wakati huu wa dirisha la Januari. ***(90min)***

### BROJA AOTA MBAWA

MATUMAINI ya West Ham kumsajili, Armando Broja, 22, yanaonekana kuwa mbali kwa Januari hii, huku Chelsea wakitaka angalau pauni milioni 50 kwa ajili ya mshambuliaji wao huyo raia wa Albania. ***(Football Insider)***

## DO… ZA SOKA MA… YA ULAYA




# UNITED YATOA OFA KUWAUZA ANTHONY NA SANCHO SAUDIA

### Yalenga kupata pauni milioni 100 kwa wote wawili, lakini...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imetoa ofa ya kuwauza Antony na Jadon Sancho kwa klabu za Saudi Arabia ili kupunguza hasara ya wachezaji hao wawili ambao hawajawa kwenye kiwango kizuri, ripoti mpya imesema.

**United ilimsajili Sancho kwa pauni milioni 73 mwaka 2021, lakini alishindwa kuwa kwenye kiwango bora kabla ya kuzozana na kocha Erik ten Hag kumfanya arejee kwa waajiri wake wa zamani Borussia Dortmund kwa mkopo wa miezi sita ambao haujumuishi chaguo la uhamisho wa kudumu.**

Antony, kwa upande wake, ameshindwa kufunga au kusaidia bao msimu huu na usajili wake wa pauni milioni 86 umeshindwa kuthibitisha kiwango chake kwenye timu.

Gazeti la Evening Standard limeripoti kwamba United iko tayari kuachana na wachezaji wote wawili na wametoa ofa ya kuwauza Antony na Sancho kwa klabu za Saudi Arabia kwa matumaini ya kupata bei ya juu zaidi.

United inasemekana kuwathaminisha Sancho na Antony kwa pauni milioni 50 kila mmoja, ili kurejesha pauni milioni 100 kwa wawili hao na 'Mashetani Wekundu' haoa watabakiwa na hasara ya pauni milioni 59.

90min iliripoti mapema mwezi huu kwamba Sancho alikuwa akilengwa na Al Ettifaq inayonolewa na Kocha Steven Gerrard wakati wa dirisha la uhamisho wa majira ya joto la 2023, lakini mazungumzo yalivunjika.

Usajili wa bei ghali Januari unatarajiwa kuwa mdogo kote Saudi Arabia, lakini kunaweza kuwa na msukumo upya wakati wa msimu wa majira ya joto.

Antony na Sancho bila shaka watakuwa miongoni mwa majina mawili mashuhuri zaidi yanayoweza kuhamishwa.

Mkurugenzi wa soka, John Murtough hivi majuzi alikutana na maofisa kadhaa wa Saudia katika Kombe la Dunia la mwezi uliopita kwa nia ya kujenga uhusiano na kuweka msingi wa uhamisho wa siku zijazo, huku mastaa kama Casemiro na Raphael Varane pia wakilengwa na klabu za huko Mashariki ya Kati.

90min inaelewa kuwa ingawa Varane anaweza kuondoka Old Trafford msimu huu wa majira ya joto wakati mkataba wake utakapomalizika, kuongezwa muda zaidi pia kunawezekana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amedokeza kwamba anatumaini kumalizia soka lake katika mojawapo ya timu tatu alizoziwakilisha hadi sasa katika maisha yake - Man United, Real Madrid na Lens - lakini maofisa wa Saudia wanabakia na matumaini ya kumshawishi kuondoka Ulaya.



# TREZEGUET: UZOEFU UTAIPA MISRI UBINGWA AFCON

**KORHOGO,** Ivory Coast

MSHAMBULIAJI Mahmoud Trezeguet, anaamini uzoefu mkubwa wa Misri unaweza kuwawezesha kutwaa ubingwa wa Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), baada ya kutinga hatua ya 16-bora kwa mbinde, Jumatatu usiku.

Winga huyo alipata tuzo ya nyota wa mchezo huo kwa kucheza bila kuchoka wakati Misri ilipotoka sare ya mabao 2-2 na Cape Verde na kufuzu kutoka Kundi B. Trezeguet, ambaye alisawazisha bao la kwanza kwa Misri, amebaki na ari na morali kubwa kuhusu nafasi yao baada ya kufuzu hatua ya 16-bora.

"Kwa miaka 10 katika timu ya taifa kwangu, hakuna kitu juu ya soka," alisema Trezeguet baada ya mechi.

"Ikimpendeza Mungu, kizazi chetu kitaondoka na kombe kwa sababu tunataka kuweka historia."

Mchezaji huyo alisema kikosi chao kilikuwa na ari ya kupambana na ubora wa Misri unaweza kuwapeleka kwenye mafanikio.

"Tulitoa kila kitu kwa ajili ya kufuzu na wachezaji wenzetu wazuri. Sasa mashindano ya kweli yanaanza," alibainisha Trezeguet.

Huku Misri ikiwa ndio bingwa wa kihistoria wa mashindano hayo ikitwaa mara saba, winga huyo anahisi uzoefu wa zamani unaweza kuwasaidia.

"Katika mechi za mtoano, uzoefu wetu utaleta mabadiliko, Mungu akipenda na tutafika mwisho," alisisitiza Trezeguet kwa kujiamini.

Baada ya kusonga mbele kama washindi wa pili wa Kundi B, nyuma ya Cape Verde, Misri inaonekana kuwa na kiwango bora kwa wakati ufaao.

Akiwa na ujuzi mkubwa wa mashindano ndani ya kikosi, Trezeguet anaamini wazi kwamba 'Mafarao' hao wanaweza kuleta ushindi mwingine kwenye Afcon mwaka huu.

## Kudus: Nimesikitishwa sana na Ghana

**ABIDJAN,** Ivory Coast

KIUNGO wa kati wa Ghana, Mohammed Kudus, hakuweza kuficha masikitiko yake kwa kutolewa kwa timu yake kwenye mashindano ya Afcon, licha ya kutangazwa kuwa mchezaji bora wa mechi Jumanne, wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 na Msumbiji.

Kudus alivutia kote, lakini kiwango chake binafsi kilifunikwa na mpambano wa ajabu wa Msumbiji na kuwaachia pointi moja.

"Nimesikitishwa sana, tulitaka ushindi, lakini haikuwa hivyo," alisema Kudus akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Ni uchungu mkubwa sana kwetu."

Mchezaji huyo wa West Ham alihisi kushindwa kwa Ghana licha ya kuwa mbele kwa mabao mawili kulitokana na kukosa umakini.

"Tulipoteza mchezo kwa kupoteza umakini katika dakika za mwisho, kama vile dhidi ya Misri pia," alilalamika mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

Hata hivyo, Kudus anaamini Ghana walionesha ubora wao usiopingika katika michuano hiyo nchini Ivory Coast.

"Tulionesha sifa nyingi hapa, lakini kupoteza mwelekeo mwishowe kulitugharimu," aliongeza.

Onyesho bora zaidi la Kudus lilikuwa mojawapo ya maeneo angavu katika kampeni ya Afcon yenye maumivu kwa Ghana.

Lakini kutajwa kuwa mchezaji bora wa mechi kunaweza kuinua ari ya nyota huyo anayechipukia kwa siku zijazo.



## Simon aridhishwa kufuzu 16 bora

**ABIDJAN,** Ivory Coast

NYOTA wa Nigeria, Moses Simon, alionesha kuridhika na ushindi mdogo wa Nigeria dhidi ya Guinea Bissau katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi ya michuano ya Mataifa Afrika, wakati walipotinga 16-bora kwa ushindi wa bao 1-0.

Simon alicheza jukumu muhimu katika goli la kujifunga la Opa Sangate, na hatimaye kuwawezesha Nigeria ambayo bado haijaonesha kiwango cha kuvutia kwenye mashindano hayo, kufuzu kwenye hatua ya mtoano.

Akiwa ameridhika na kiwango chake cha sasa, Simon anaamini kuwa amefikia wakati bora uliokuwa unatarajiwa kuichezea Super Eagles hao.

"Katika hali nzuri, kimwili na kiakili, ninajaribu mambo mengi, hata kama matokeo hayawiani na nia yangu kila wakati," alisema.

"Ninajiweka mahali ninapohitajika. Lengo letu la msingi lilikuwa kupata ushindi, kuhakikisha tunafuzu kwa hatua ya mtoano na kuepuka hesabu ngumu," aliongeza.

Baada ya kunyakua nafasi ya pili katika Kundi A kwa pointi saba, Nigeria inapanga kukabiliana na timu iliyo nafasi ya pili Kundi C Januari 27 katika Uwanja wa Felix Houphouet Boigny mjini Abidjan.

"Kila timu ni hatari, tunahitaji kupumzika vizuri na kuanza upya," alibainisha.

HABARI MICHEZO

# AZAM FC YAJIGAMBA KUTISHA RAUNDI YA PILI

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC umesema mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara watakuja kivingine baada ya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Youssouph Dabo, kupata mwarobaini wa madhaifu yaliyojitokeza katika mechi za mwanzo za duru la pili la Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kikosi cha Azam FC kimeingia kambini leo (jana), Azam Complex, Chamazi, na leo au kesho kinatarajia kwenda visiwani Zanzibar kwa ajili ya kambi ya siku kadhaa kabla ya kurejea kwa ligi hiyo ambayo ipo kwenye mapumziko kupisha Fainali za Mataifa ya Afrika, AFCON.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Hashim Ibwe, alisema timu yao imeingia kambini jana na wachezaji wote waliowasajili, na wapo tayari kwa ajili ya kuendelea walipoishia katika mechi za mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo.

**Alisema tayari kocha Dabo ameshawasili nchini akitokea mapumzikoni Ufaransa kuona familia yake na amekuja kuvingine baada ya kupata matibabu ya matatizo ya timu yake.**

"Kocha Dabo alikuwa mapumziko, lakini pia kuongeza ujuzi na kuja na dawa ya kutibu matatizo ya timu yetu yaliyojitokeza kwenye mechi za mzunguko wa kwanza, tunaamini kurejea kwake kila kitu kitakuwa vizuri," alisema Ibwe.

Aliongeza kuwa katika dirisha dogo la usajili waliamua kuongeza wachezaji wachache ikiwamo kuimarisha safu ya ushambuliaji kwa kuinasa saini ya Franklin Navarro huku safu ya ulinzi wakiwasajili Yeison Fuentes na kipa Mohammed Mustapha.

MWENDO...



Mshambuliaji wa Nigeria, Samuel Chukwueze, akiambaa na mpira kuelekea langoni mwa Guinea-Bissau, katika mechi ya Kundi A ya Fainali za Mataifa ya Afrika iliyopigwa katika Uwanja wa Felix Houphouet-Boigny, Abidjan nchini Ivory Coast juzi usiku. Nigeria ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Simba kufyeka tena wachezaji

INATOKA UK. 24

KMC, Jean Baleke aliyerejea TP Mazembe, na Moses Phiri ambaye ameeleka Power Dynamos ya Zambia.

Timu hiyo imewasajili Babacar Sarr kama mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake na Klabu ya US Monastir ya Tunisia, Salehe Karabaka kutoka JKU ya Zanzibar, Omar Jobe kutoka Zhenis ya Kazakhstan, Freddy Michael Kouablan, akisajiliwa kutoka Green Eagles ya Zambia, na Ladack Chasambi kutoka Mtibwa Sugar.

Try Again alisema Benchikha ndiye aliyependekeza wachezaji waliosajiliwa na walioachwa, huku wengine wakiponea kwenye Kombe la Mapinduzi.

„Usajili huu ni mapendekezo ya mwalimu alitupa ripoti ya wachezaji wangapi tuwaache na wangapi tusajili na akatoa maelekezo ya maeneo ya kusajili na hata majina ya wachezaji akisema namtaka huyu.

„Kwa hiyo niseme tu kuwa usajili wetu umezingatia maekezo ya mwalimu na baadhi ya aliosema tuwaache wamekwenda kuponea Kombe la Mapinduzi, Zanzibar ambako baada ya kufanye vema akabadili msimamo wake na kuwabakisha kikosini," alisema.

Aliongeza kuwa watakaojituma kwenye nusu msimu huu wataendelea kuwapo, lakini watakaoonekana wanacheza chini ya kiwango watawaondoa hata kama walisajiliwa kipindi cha dirisha dogo.

„Awali, tuliwahi kusema kuwa mchezaji ambaye haonyeshi kiwango cha kujituma basi tutaachana naye, ndivyo itakavyokuwa na mwalimu wetu amebariki hilo, hata kama tulimsajili dirisha dogo ataondoka tu, msimu ujao tunataka kutengeneze kikosi cha wachezaji wenye uwezo mkubwa, wapambanaji na wenye nidhamu," alisema Try Again.

## *Stars machozi, jasho na damu*

INATOKA UK. 24

"Nilisema kuwa mechi iliyopita tuliangushwa na umakini hasa baada ya wenzetu kuwa pungufu, lakini tumerejea kwenye uwanja wa mazoezi na kuyafanyia kazi mapungufu yote, nafikiri kesho (leo), tutakuwa vizuri zaidi kuliko mechi zingine zote tulizopita na ili tusonge mbele ni lazima tushinde mechi ya leo, kila mtu anajua hilo hata wachezaji wanalijua hilo, na wameahidi kupambana kwa uwezo wao wote," alisema kocha huyo.

Nahodha wa timu hiyo, Mbwana Samatta, alisema kuwa ni lazima mechi ya leo wapambane hadi tone la mwisho la damu ili kupata ushindi, kwa sababu ni huo tu utakaowawezesha kusonga mbele na si vinginevyo.

"Hatuna kingine, tuna mchezo mmoja tu ambao ni huu, tunatakiwa tushinde kwa hiyo kila mchezaji ataingia kuhakikisha kwanza tunapata ushindi, ili tungalie sasa kama tunaweza kusonga mbele kwenye hatua nyingine," alisema Samatta.

Katika mechi ya kwanza, Stars ilichapwa mabao 3-0 dhidi ya Morocco, kabla ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Zambia.

Stars inahitaji ushindi ili ifikishe pointi nne, huku pia ikiomba Morocco iifunge Zambia au kutoka nayo sare, na kama itakuwa hivyo moja kwa moja itakuwa imetinga hatua ya 16 bora.

Mpaka sasa inashika mkia kwenye kundi lake ikiwa na pointi moja, Morocco ikiwa kileleni na pointi nne, DR Congo na Zambia zina pointi mbili kila moja na zikifanana kwa kila kitu, ingawa Wakongomani wanakaa nafasi ya pili kwa sababu ya alfabeti tu.

## Gamondi jicho kwa Nzengeli

INATOKA UK. 24

mchezaji tegemeo zaidi aliyebaki, wengine wakiwa kwenye vikosi vya timu zao za taifa zinazoshiriki AFCON nchini Ivory Coast. Akizungumza na Nipashe jana, Kocha huyo alisema kuna vita nyingine uwanjani ya kusaka ushindi kwenye mashindano yanayowakabili kwa kuwa ni muhimu kufanya vizuri na kikubwa ni kupata ushindi uwanjani.

Alisema wachezaji wake wote ni muhimu kuwa fiti, hasa safu ya kiungo na ushambuliaji kwa ajili ya kuwa kwenye kiwango bora ndani ya timu, kuelekea katika mashindano ambayo wanashiriki.

"Kila mchezaji anatambua umuhimu wa kufanya kazi kwa umakini na kutimiza majukumu ambayo yapo na inawezekana kuwa katika ubora kwenye mechi ambazo tunacheza .

"Tunahitaji kufanya vizuri katika mashindano hayo matatu yaliyopo mbele yetu, kwanza kutetea mataji yetu ya ubingwa wa ligi na FA, pamoja na kuvuka kwenye robo na kwenda nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa, ambayo inawezekana wachezaji wakipambana," alisema kocha huyo.

# Michezo

Jumatano Januari 24, 2024

Nipashe




‘Uzoefu utaipa Misri ubingwa Afcon’ UKURASA 22



Mshambuliaji na Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, akiwa mazoezini nchini Ivory Coast. Leo watashuka dimbani kukamilisha mechi yao ya hatua ya makundi ya Afcon dhidi ya DR Congo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Taifa Stars machozi, jasho na damu leo*

## Morocco, Samatta wafunguka, morali ya wachezaji ipo juu, waitaka...

**Na Adam Fungamwango**

HATMA ya Timu ya Taifa ya Tanzania kusonga mbele kwenye Fainali za Mataifa ya Afrika itajulikana leo itakaposhuka Uwanja wa Amadou Gon Coulibaly nchini Ivory Coast, saa tano usiku kucheza dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, huku Kaimu Kocha Mkuu Hemed Morocco akiahidi timu kupambana kwa machozi, jasho na damu kuhakikisha inapata ushindi.

Ni mechi ya mwisho kwenye Kundi F, ambapo matokeo ya mchezo huo na mingine itakayochezwa muda mmoja kati ya Zambia na Morocco, kwenye Uwanja wa Laurent Pokou, San-Pedro, ndiyo itaamua nani asonge mbele na nani abaki.

Timu mbili zitakazomaliza zikiwa juu ya msimamo zitatinga hatua ya 16 bora, ingawa pia kuna timu nne zitakazokuwa na uwiano mzuri wa matokeo na kushika nafasi ya tatu, zitakwenda hatua hiyo kwa mtindo wa mshindwa bora (best looser).

**Morocco amesema mechi ya leo dhidi ya DR Congo haitokuwa rahisi kwani ni timu ngumu, lakini na wao pia wamejiandaa kwa hilo.**

INAENDELEA UK. 23

# Gamondi jicho kwa Nzengeli

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema anahitaji wachezaji wake muhimu anaowategemea kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa na Ligi Kuu kuwa fiti, hivyo bado anaendelea na mazoezi ya fiziki, huku kiungo mshambuliaji Maxi Nzengeli akionekana kuangaliwa zaidi katika zoezi hilo.

Amesema licha ya kuwa na wachezaji pungufu wengine wakiwa katika majukumu ya timu za Taifa kwa walikuwapo wataendelea kuongezewa dozi ya mazoezi kulingana na umuhimu wa mashindano yaliyopo mbele yao ikiwamo Kombe la FA.

Kikosi cha Yanga kinaendelea kujifua na mazoezi katika Uwanja wa Avic Town, Kigamboni na kinatarajia kucheza mechi ya kirafiki wikiendi hii dhidi ya JKU FC ya visiwani Zanzibar, jijini Dar es Salaam.

Nzengeli alionekana kufuatiliwa zaidi kwa sababu ni

INAENDELEA UK. 23

# Simba kuanza tena kufyeka wachezaji

**Na Adam Fungamwnago**

KLABU ya Simba imesema haijamaliza kuondoa wachezaji walioshuka viwango, au wote wasiojituma kwenye kikosi hicho na kutoa angalizo kuwa yeyote asiyefanya hivyo ataachwa mwishoni mwa msimu hata kama alisajiliwa kipindi cha dirisha dogo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Klabu hiyo, Salim Abdallah ‚Try Again‘, amesema zoezi la kufyeka wachezaji wote wavivu, walioshuka viwango na wasiojituma bado linaendelea na linafanywa na Kocha Mkuu Abdelhak Benchikha kwa kushirikiana na viongozi, hivyo kuwataka wachezaji wote waliopo sasa wafanye kazi ya kuipambania Simba na si vinginevyo.

„Dirisha kubwa linakuja, nasisitiza kusema tena huu tena si mjadala, hatutaangalia sura wala jina la mtu au wewe ni maarufu kiasi gani, au wapenzi wanakukubali kiasi gani, tunachotaka sisi ni kitu gani unatupa kwenye klabu yetu.

„Mchezaji umeajiriwa kazi yako ni kufanya kazi ya kuiletea ushindi Simba, ukishindwa tunakuondoa tunaweka mwingine kwa hiyo tutaendelea na panga hili kama kawaida, hivi sasa tunalinoa kwa ajili ya kufanya kazi mwishoni mwa msimu.

„Nitoe wito kwa wachezaji wote wafanye kazi ya kuisaidia klabu ya Simba, la sivyo ‚thank you‘ itamhusu mwishoni mwa ligi,“ alisisitiza kiongozi huyo.

Tayari Simba imeshawatoa baadhi ya wachezaji na kuwapeleka wengine kwa mkopo mwishoni mwa dirisha dogo la usajili.

Wachezaji hao ni Jimmson Mwanuke na Nassor Kapama waliokwenda Mtibwa Sugar, Shaaban Chilunda akienda

INAENDELEA UK. 23



Benchikha

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >